# Nipashe

Jumatatu Januari 25, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580471

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11

**Sababu** Day care 33 kufungiwa na serikali



UKURASA 3

**Askari** SUMA-JKT anayedaiwa kujeruhi apewa kibano

UKURASA 5

# Wenye hoteli walia kukamuliwa na mabasi

UKURASA 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**POLISI SITA, MTENDAJI KORTINI MADAI RUSHWA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya...

UKURASA WA 5

**MAKAMU AZIHIMIZA MAHAKAMA KUTOA HAKI**

MAKAMU wa Rais, Samia Hassan, amezitaka mahakama kuhakikisha...





Ofisa Ustawi wa Jamii Mkuu kutoka Wizara ya Afya Idara Kuu ya Maendeleo, Miriam Luka, akisitisha huduma katika moja ya kituo cha kulelea watoto mchana kilichopo katika Manispaa ya Jiji la Tanga kwa kutoa huduma ya malezi kwa watoto bila kusajiliwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Zanzibar yajipanga kwa vivutio vipya utalii



UKURASA 4



## Wilaya sita marufuku kula kitimoto

UKURASA 3





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play

App Store



**MICHEZO** **DIDIER AMRITHI SVEN SIMBA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Polisi sita, mtendaji kortini madai ya rushwa

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Igunga, mkoani Tabora imewapandisha kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mfawidhi wilaya ya Igunga, askari sita wa Jeshi la Polisi wilayani Igunga na Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Isakamaliwa kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 8,450,000.

Wanadaiwa kupokea fedha hizo kutoka kwa wazee wawili wa Kijiji cha Isakamaliwa, akiwamo mzee mwenye umri wa miaka 85.

Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU) Wilaya ya Igunga, Mazengo Joseph aliwataja askari hao pamoja na Ofisa Mtendaji huyo kuwa ni Ass.INSP. Frank Matiku (36), PC.Raphael Charles (31),D/CPL. Paul Bushishi (49), DC Lucas Nyoni(31), PC.Lome Laizer(39),CPL. Charles Zacharia(45) na Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Isakamaliwa, Edward Kitenya (42).

Mbele ya Hakimu wa Wilaya ya Igunga, Eddah Kahindi, ilidaiwa katika shtaka la kwanza la kuomba rushwa kutoka kwa Nkende Ngaka, Juni,12,mwaka 2019 saa nne asubuhi katika Kijiji cha Isakamaliwa askari hao waliomba Sh. milioni nane ili wasimchukulie hatua baba yake aliyetambulika kwa jina la Ngaka Mataluma kwa madai ya kujihusisha na tiba asili bila kuwa na kibali.

Shitala lingine ni la kukutwa na silaha kinyume cha sheria na taratibu.

Shitaka la tatu linalowakabili washitakiwa wote ni la kuomba rushwa ya Sh. 450,000 kutoka kwa Jilumba Hamka Habi. Ilidaiwa kwamba katika tarehe hiyo na mwezi huo huo, mwaka 2019 waliomba kiasi hicho ili wasimchukulie hatua kwa kukutwa na nyara za serikali.

Hata hivyo baada ya washtakiwa hao kusomewa mashitaka hayo walikana kutenda, na upande wa mashtaka ulidai kuwa upelelezi umekamilika na unatarajia kupeleka mashahidi 18.

Washtakiwa wote wapo nje kwa dhamana ya maandishi ya shilingi milioni nane kila mmoja hadi kesi hiyo itakapoanza kusikilizwa Aprili 17 na 18, mwaka huu.

# Wenye hoteli walia kukamuliwa na mabasi

**Na Elizabeth Zaya**

SIKU chache baada ya gazeti hili kuibua taarifa za namna abiria wanavyolanguliwa bei ya vyakula na vinywaji katika hoteli za barabarani, wamiliki wa hotel hizo wameibua mapya na kueleza wanavyopata hasara.

Nipashe ilifanya mahojiano na wamiliki wa hoteli zilizopo mkoani Morogoro ambao hawakutaka kutaja majina yao na kueleza kuwa hoteli zao ziko hatarini kufungwa, kutokana na gharama kubwa wanazotumia kuwalipa posho madereva ili wawapelekee wateja (abiria).

Wakizungumza na Nipashe kwa sharti la kutokutajwa majina yao, wanasema kwa kipindi kirefu wamekuwa kama watumwa kwa kuwalipa madereva wa mabasi hayo ya mikoani posho kwa makubaliano ya kupelekewa wateja ambao ni abiria wanaokuwa wanatumia mabasi yao kusafiri.

Walisema mbali na kuwalipa posho, pia wamekuwa wakiwagharamia kwa chakula na vinywaji, madereva na wahudumu wote wanaokuwa kwenye kila gari, hivyo kujikuta wakitumia gharama kubwa, huku wakishindwa kupata faida kama wanavyokuwa wametarajia.

Mmojawapo wa wamiliki wa miongoni mwa hoteli hizo iliyopo katika eneo la Msamvu Manispaa ya Morogoro, alisema gharama anazotumia kulipa madereva na kuwahudumia ni kubwa kuliko kile wanachokipata.

"Ni kweli wengi wetu tuliwekeza katika biashara hii kwa matumaini makubwa tukitarajia kwamba tutafaidika, lakini tunachokiona na tunachokutana nacho ni tofauti na matarajio," alisema na kuendelea:

"Hii ni biashara kama zilivyo nyingine na kama kawaida ili ufanye vizuri katika biashara yako lazima uzungumze na watu na ujue kutafuta wateja wapya, ndicho tulichokifanya kwa madereva, lakini sasa tunaona hili limekuwa tatizo."

"Kwa mfano katika hoteli yangu, kwa siku gari zinaweza kuingia hata 50, na kila gari wanataka niwalipe Sh. 40,000, hapo dereva na wahudumu wake wanakula chakula na kupata vinywaji bure na gari lingine wanakuwa watatu hadi wanne kwa ujumla wao, kwa hiyo fedha najikuta nalipa zaidi ya Sh. milioni 2 kwa siku moja tu, kwa mwezi ni zaidi ya Sh. milioni 60."

Anasema wakati mwingine wanalipa fedha hizo kwa madereva, lakini abiria wanapoingia wanaishia kununua biskuti, maji au soda pekee na wachache wanaonunua chakula.

"Kwa hiyo unapata hasara badala ya faida na ukiwaambia madereva, wanasema makubaliano yao si kuangalia ni abiria wangapi wamekula na wangapi hawajala. Unavumilia ukiamini labda kesho hali itakuwa nzuri, lakini ni yaleyale," alisema na kuongeza:

"Hali hiyo inaweza kufululiza hivyo hadi siku tano au nne ndani ya wiki moja, siku mbili au tatu tu ndio angalau unabahatisha kupata kidogo ambayo nayo hailingani na kile unachotoa ukipiga hesabu."

Mmiliki mwingine ambaye alisema hoteli yake iko kilomita tano kutoka stendi ya Msamvu, alisema wakati anawekeza katika biashara hiyo alikopa fedha benki akiamini itamlipa, lakini matarajio yake yamekuwa tofauti.

"Taarifa ambayo Nipashe mliiandika katika gazeti lenu kuhusu madereva wanaosafirisha abiria kwenda mikoani kupewa posho na wenye hoteli ni kweli, tunafanya hivyo kuvutia biashara zetu, lakini mpaka hivi tunaongea imetuelemea, hali si shwari, ninavyozungumza hapa ninadaiwa na benki na sielewi namalizaje hili deni, maana biashara hailipi kabisa,"alisema.

"Ninapata shida kuwalipa hata wafanyakazi wa hoteli ili tu fedha ninayopata niwalipe madereva kwa sababu usipofanya hivyo hawaleti abiria, lakini sasa kinachotokea unajikuta mwisho wa siku unawahangaikia wao tu, wewe haufaidiki. Hii biashara ni zaidi ya 'stress' na wengine tulijiingiza huku hatukujua kama tutakutana na haya."

Alisema ameamua kutangaza kwa ajili ya kumwachia mwekezaji mwingine.

"Mwaka jana Novemba baada ya kuona hali ni ngumu zaidi, niliamua kuifunga kwanza kwa wiki mbili, halafu Desemba mwanzoni nikafungua tena nikitega wale wanaosafiri mwishoni mwa mwaka, lakini kwa sasa hali imerudi vilevile na siitaki tena hii biasahara, nimeamua kutangaza kumwachia mwekezaji mwingine atakayeona yuko tayari kuiendesha mimi nimeelemewa, na mpaka sasa sijapata mtu,"alisema.

Mmiliki mwingine wa hoteli katika barabara ya kuelekea mkoani Mtwara, alisema mwanzoni wakati anaanza alikuwa hajagundua mbinu hiyo ya kuwalipa posho madereva, hivyo magari yalikuwa hayaingii katika hoteli yake.

"Mwanzoni kabisa wakati naanza nilijua kwamba kwa sababu iko barabarani magari yataingia tu, lakini haikuwa hivyo, kumbe huwa wanaambizana na baadhi ya madereva walinifuata wakaniambia namna wenzangu wanavyofanya ikabidi na mimi nifanye hivyo,"alieleza.

"Nilichogundua ni kwamba, kuwapa posho kidogo madereva siyo jambo baya sana, lakini kiwango wanachodai ni kikubwa sana hasa wenye mabasi haya ya 'luxury', yaani wangetupunguzia tukawapa hata Sh.10,000 kila gari au wakasema tukawapa chakula tu tungepata faida, lakini wengine wanataka uwalipe hadi Sh. 50,000 kwa siku usipowapa tu mabasi yao hawaleti,"alisema.

"Siyo madereva tu, hata baadhi ya wamiliki hasa wenye abiria wale wa viwango fulani vya juu, wanataka na wao tuwalipe hata Sh. 20,000 kila siku, yaani hii biashara ni ngumu sana na usipofanya hivyo hawaingizi basi kwako."

"Mahoteli haya ya barabarani ambayo yanategemea abiria, mengi sana yanakufa kwa ajili hiyo na kama hili halitajadiliwa na kupatiwa ufumbuzi wengi sana watajiondoa katika uwekezaji huu maana haina faida kabisa na tunashindwa kurejesha mikopo benki tunayochukua kwa ajili ya biashara hii."

Alisema kipindi ambacho wanapata faida kidogo ni cha kufunga na kufunguliwa kwa shule.

"Wakati wa kufunga au kufunguliwa shule ndio kipindi ambacho angalau huwa tunapata faida kidogo, wanafunzi ndio huwa wanapenda kulakula,"alisema.

Alishauri kwamba ni vema serikali ingeweka utaratibu wa kupanga upya utaratibu wa kuziorodhesha hoteli zinazotoa huduma kwa wasafiri wa barabarani na kupanga idadi ya mabasi yanayotakiwa kuingia kila siku katika hoteli.

"Mimi naamini serikali ikipanga kwamba basi kadhaa za njia A au B zinatakiwa kuingia kupata huduma katika hoteli C, hata huduma nyingine za usafi zitaboreshwa zaidi, siyo kama ilivyo sasa, hoteli moja tu ndio wateja wanalundikana humo, bila kujali hata kama ni kuchafu eti kwa sababu tu madereva wamelipwa , hii ni hatari hata kwa afya yao,"alishauri.

"Hata hili wanalolalamikia abiria la kwamba hoteli zinaweka bei kubwa za vyakula, nalo wanaweza kuliwekea bei elekezi, kikubwa kwa sasa waitishe mjadala ili tujipange upya, la sivyo wote tutakimbia."

Januari 18 mwaka huu, Nipashe lilichapisha habari iliyokuwa ikizungumzia abiria wakilalamika viwango vya juu vya bei ya chakula wanavyochajiwa katika hoteli hizo za barabarani na ubovu wa huduma nyinginezo ikiwamo za maliwato.

Katika habari hiyo, Chama cha kutetea abiria(CHAKUA), Chama cha Wamiliki wa Mabasi(TABOA) walikiri kuwapo kwa tatizo hilo.

Pia, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini(LATRA), ilisema sheria na taratibu zinazosimamia sekta hiyo, hazitoi mwanya wa kudhibiti bei za vyakula na kuahidi kwamba suala hilo si la kuachwa hivyo lilivyo na kwamba kuna haja ya kuangalia upya namna ya kulitatua kwa kushirikiana mamlaka nyingine."




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizindua Mwongozo wa Uwekezaji mjini Iringa kwenye ukumbi wa Chuo Kikuu cha Mkwawa mjini humo, Januari 23, 2021. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi na kulia ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo. **Habari Uk 7.** **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

## Day Care 33 zafungwa Tanga

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

SERIKALI imesema kuwa imebaini nusu ya vituo vya kulelea Watoto Mchana (Day Care Centers), vinaendeshwa kinyemela pasipo taratibu muhimu za kisheria.

Hayo yalibainika mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya Maofisa kutoka Wizara ya Afya-Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, kubaini kuwa kati ya vituo 68 vya malezi ya watoto mchana, vituo 33 pekee ndivyo vyenye usajili wa kutoa huduma hizo kisheria.

Kufuatia hali hiyo, timu ya Ukaguzi ikiongozwa na Mwakilishi wa Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Miriam Luka, ikalazimika kufunga vituo kadhaa vilivyokithiri na kuvitaka kufuata Sheria na Kanuni za uanzishwaji wa Vituo vya Malezi kwa watoto wadogo mchana.

Akizungumza kwa niaba ya Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Ofisa Ustawi wa Jamii Mkuu kutoka Wizara ya Afya-Idara Kuu ya Maendeleo, Luka alisema vituo vya malezi kwa watoto mchana vinaendeshwa kwa mujibu wa taratibu na kanuni zilizopo chini ya Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 inayoelekeza namna ya endeshaji wa vituo hivyo.

"Mimi nazungumza kwa niaba ya Kamishna wa Ustawi wa Jamii hivi vituo havifai kwa kutoa huduma kwa watoto wetu, mazingira hayafai kabisa tafuteni sehemu sahihi ndiyo muanzishe hivi vituo,"alisema.

Awali, Katibu Mkuu Wizara ya Afya-Idara Kuu ya Maendeleo, Dk. John Jingu, akiwa katika kikao kazi na Maofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Tanga, aliwaagiza Maofisa hao nchini kukagua na kufuatilia uendeshaji wa vituo hivyo na kuona jinsi wanavyotoa huduma za malezi kwa watoto.

Aidha, aliwataka Maofisa Ustawi wa Jamii nchini kuhakikisha wanasimamia uendeshwaji wa Vituo vya Malezi na Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto mchana (Day Care Centers), ikiwamo kukagua maeneo na huduma zinazotolewa na vituo hivyo ili vitoe huduma stahiki kwa watoto nchini.

"Tusimamie hivi vituo kwa ukaribu watoto wetu wanaenda huko tuangalie mazingira yake yakidhi vigezo vilivyowekwa ili tuweze kumpatia mtoto malezi yanayostahili," alisisitiza.

Kwa mujibu wa Dk. Jingu, Kada ya Ustawi wa Jamii ni muhimu katika kuhakikisha Jamii inajengeka vizuri na kutatua changamoto za jamii husika hasa katika masuala ya saikolojia.

Aidha, alikemea uanzishwaji holela wa vituo vya malezi kwa watoto wadogo bila kuzingatia Sheria na Kanuni zilizopo na kuwataka wamiliki wa vituo hivyo kuzingatia sheria, ili kuepusha changamoto zinazoweza kujitokeza katika uendeshaji wa Vituo hivyo.

# Kitimoto marufuku wilaya sita

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amepiga marufuku ulaji na uuzaji wa nyama ya nguruwe kwenye wilaya sita za mikoa ya Kanda ya Ziwa, kutokana na uwapo wa ugonjwa wa homa ya nguruwe ambao umesababisha vifo vya nguruwe 1,500.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kuhusu kukabiliana na ugonjwa huo, Waziri huyo alisema hatua hiyo inalenga kudhibiti ugonjwa huo unaoenea kwa kasi ambapo wilaya za Mbogwe, Sengerema, Geita, Misungwi, Kyerwa na Kahama.

"Nawasihi wananchi kwenye maeneo haya wasile nyama ya nguruwe, ni kitu kigumu kidogo, ili tudhibiti ugonjwa huu, kama mtu akila nguruwe ambaye ameambukizwa huu ugonjwa watatumika kama chombo cha kusafirisha ugonjwa huu kwa wengine,"alisema.

Alikemea tabia ya kuchinja ovyo nguruwe kwa kuwa inasababisha virusi vya nguruwe kuenea kwenye maeneo mengine.

"Kirusi kikiingia kwenye banda kinaua nguruwe wote kwa haraka, tudhibiti ugonjwa huu kwa kuzingatia haya," alisema.

Aliagiza kuepuka kusafirisha nguruwe na mazao yake na kuingia kwenye maeneo yaliyoathirika na ugonjwa huo na kwamba hali hiyo itasaidia kudhibiti ugonjwa huo.

"Pia wananchi waepuke kununua nguruwe au mazao yao kutoka maeneo yaliyoathirika kwa kuwa maeneo hayo bei ya nguruwe imeshuka, wafugaji wasiruhusu wachinjaji au wafanyabishara kuingia katika mabanda kuchagua nguruwe kwa sababu anasababisha kusambaza ugonjwa,"alisema.

Aliwaasa kuepuka kulisha nguruwe mabaki ya nguruwe wanayokusanya kutoka mahotelini au maeneo ambayo inaliwa nyama ya nguruwe.

Ndaki alisema nguruwe hao 1,500 waliokufa wamesababisha hasara kwa wafugaji ya Sh. milioni 375 huku Wilaya ya Kahama ikionekana kuathirika zaidi ambapo nguruwe 909 wamekufa.

Alisema kama ukifanyika uzembe ugonjwa huo utaenea nchi nzima kwa haraka, na kwamba serikali haina nia mbaya ya kuua biashara hiyo bali ni hatua za kudhibiti ugonjwa huo.

"Tumeendelea kuchukua hatua kwanza tumeagiza timu ya wataalamu wa Wizara ili kwenda huko na pia Wakala wetu wa Maabara tumewaagiza wafanye uchunguzi waende huko na tumeshirikisha Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), lakini pia tumewashirikisha Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO),"alisema.



Katibu wa Mpango Mkakati wa Serikali kitaifa wa kutokomeza matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA) Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Aisha Omari, akiwataka watoto katika kijiji cha Shilabela, wilayani humo, wapaze sauti za kupinga matukio ya ukatili dhidi yao kupitia kwa viongozi wa mabaraza ya watoto zikiwamo njama za kuozeshwa ndoa za utotoni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zanzibar yajipanga vivutio vipya vya utalii

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar, imesema inajipanga kuwa na vivutio vipya vingi vya utalii ili kumwezesha mtalii anapokuja nchini kutumia muda mrefu na kupata hamu kurudi tena kutembelea vivutio vingine.

Pia, inatarajia kuboresha vivutio hivyo ikiwamo mambo ya kale kwa kushirikiana na sekta binafsi kuwekeza, ili kuimarisha na kuboresha vivutio hivyo katika mkakati wa kuongeza idadi ya watalii visiwani humo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari wa IPP Media, Mikocheni, jijini Dar es Salaam jana, katika mahojiano maalumu, Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Leila Mohamed Mussa, alisema Zanzibar imejipanga kikamilifu katika kuhakikisha utalii unaliingizia taifa hilo fedha nyingi za kigeni.

"Uchumi wa Zanzibar unategemea utalii kwa asilimia 28 na asilimia 80 ya fedha za kigeni zinatokana na utalii... Corona ilituathiri sana kiasi cha kukosa watalii kabisa ambao wengi walitoka Ulaya Mashariki, kwa sasa tunapata watalii wengi kutoka Ulaya Magharibi," alibainisha.

"Baada ya Corona kupiga nchi tunazozitegemea kwenye utalii tulikuja na mpango wa kuboresha, kufufua kwa kuhakikisha tunapata watalii wengi wa mataifa ambayo hayajaathiriwa sana, na tulifanikiwa kwa kiasi kikubwa ndiyo maana kwa sasa tuna watalii wengi kutoka Ulaya Magharibi," alifafanua.

Alisema Zanzibar inategemea utalii wa fukwe ambazo ni nzuri, lakini bado hazijaendelezwa vizuri kwa ajili ya kutumika ipasavyo, na kwa sasa serikali iko katika mpango wa kuziboresha ikiwamo kuunganisha vivutio vingine kama utalii wa misitu na kumwezesha mtalii kuwa na vivutio vingi na kupata muda mrefu wa kuvitembelea.

"Tunataka mtalii akifika Zanzibar asiishie ufukweni tu bali aweze kwenda sehemu nyingine, tunaongeza ubora wa vivutio vingine kama mbinu ya kuongeza watalii na kuwafanya waende na kurudi," alisema Waziri Leila.

Aidha, alisema kwa sasa wanashirikiana na sekta binafsi na ametangaza fursa za watu kuwekeza katika vivutio vya kihistoria huku kipaumbele kikiwa ni kutoa ajira kwa wazawa, na kwamba kwa mwaka jana walipokea watalii 260,533.

Kwa mujibu wa Waziri Leila, wizara yake imejipanga kufikisha watalii milioni nane na ajira 300,000 mwaka 2025 kwa kuongeza vivutio vipya na kuboresha miundombinu.

**Soma zaidi mahojiano Uk. 4**

# Zanzibar kuongeza vivutio vya utalii visivyojulikana

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale wa Zanzibar, Leila Mohamed Mussa (pichani), ameelezea mikakati inayofanywa na serikali kuboresha sekta ya utalii visiwani humo kwa kuongeza vivutio visivyojulikana ili kuongeza idadi ya watalii nchini. Fuatilia mahojiano haya:



**Swali: Uchumi wa Zanzibar unategemea sana sekta ya utalii, mlipuko wa virusi vya Corona umeathiri kwa kiasi gani sekta hii.**

**Jibu:** Ni kweli Zanzibar kwa asilimia kubwa tunategemea sekta ya utalii, tunasema ni sekta mama. Karibu asilimia 28 ya GPD ya uchumi inategemea utalii na fedha za kigeni zaidi ya asilimia 80 zinatokana na mchango wa sekta ya utalii. Kipindi cha Corona Zanzibar tuliathirika sana, ilifika kipindi hoteli zilifungwa, viwanja vya ndege vilifunga, bandari zilifungwa, sisi wenyewe ilibidi tufunge. Ilifika wakati income (kipato) tuliteteteka sana hatuna kabisa kipato mpaka salary (mshahara) ikawa changamoto kwa serikali. Wageni tukawa tunapata 300 tu kwa mwezi. Kipindi kile cha lockdown (kujifungia) Wizara ya Utalii haikukaa tu, ilikuja na recovering plan (mipango ya ufufuaji), lazima tujipange ili hali itakapoisha turudi katika hali ya kawaida na kipindi kile watu wengi walikosa ajira, si kwa hoteli tu hata wananchi wa kawaida. Kila mmoja kwa nafasi yake aliathirika na hata huduma muhimu ziliathirika kama umeme na maji.

Hata hivyo, katika 'recovering plan', tulifanya mikutano ya kimkakati kwa kufanya mawasiliano na balozi mbalimbali duniani kuangalia sehemu gani imeathirika sana na corona na wakati ule soko letu kubwa lilikuwa Ulaya Magharibi, nchi kama Uingereza, Canada, Marekani na Italia, ziliathirika sana. Tulioopona nchi za Ulaya Mashariki hazikuathirika sana, ikabidi tuhamie huko kutangaza soko letu la utalii, nchi kama Poland na nyingine, ndiyo maana soko letu limehamia huko. Unaona sasa mashirika mengi sana mageni ambayo yalikuwa hayana safari za Zanzibar yanakuja. Tulikuwa katika hali mbaya sana. Asante Mungu sasa wamerudi na biashara Zanzibar inaendelea.

**Swali: Zanzibar inasifika kwa kuwa na fukwe nzuri na kubwa, je, ni kwa kiasi gani utalii wa fukwe umeendelezwa na umesaidia kiasi gani kuongeza idadi ya watalii na mapato visiwani humo.**

**Jibu:** Zanzibar is a beautiful island (kisiwa kizuri) it's a romantic, natural beauty (kina uzuri wa asili), ukiingia tu unavutiwa na mandhari yake, ukiingia Zanzibar unatokea kwenye fukwe ya pale Forodhani, nakubali kuwa fukwe haziendelezwa kwa potential (uwezo) ya uvutiaji kwa utalii. Serikali katika awamu ya nane imeamua kujipanga kuhakikisha mtalii atakapofika Zanzibar anapata vivutio mbalimbali kama michezo ya kwenye maji, ngoma za asili na sehemu za kitamaduni za asili, badala tu ya kuangalia fukwe anapotoka anapata ladha tofauti.

Tunataka mtalii apate vivutio vingine, tunayo misitu kama ya Jozani na Ngezi, ambayo tutaiongezea ubora na viwango ili badala ya mtalii anapoingia kukutana na kitu kimoja pekee, apate vitu mbalimbali na kuwa na kumbukumbu nzuri ya pale anapokwenda.

Zanzibar tunajitangaza sana kwenye fukwe, mara nyingi watalii wanapokuja kwenye fukwe na wakishaziona anakuwa hana hamu ya kurudi tena. Kwa hiyo awamu ya nane itatangaza vyanzo vyetu vya historia, mtalii asiishie kwenye fukwe tu, atembelee vyanzo hivyo kama House of Wonders (jumba la maajabu), ambalo ndiyo alama ya Zanzibar. Hivi vyanzo vya historia, serikali itafanyakazi pamoja na sekta binafsi kwa kukodisha, kuingia ubia au kupangisha, katika maeneo yanayovutia sana. Hivyo lazima tuviboreshe viwe katika hali ya kisasa ili watalii wapate kwenda. Kuna nchi nyingi ambazo hazina fukwe, lakini maeneo yao ya kihistoria yanawaingizia watalii wengi. Kwa mfano nchi ya Misri zile pyramids zinawaingizia mapato mengi.

Uzoefu unaonyesha watalii wanapokuja hawana utamaduni wa kurudi, labda hatuwapatii huduma nzuri kwa sababu hatuwapi vitu vya kutosha. Kuna sehemu za kihistoria kama Mwinyi Mkuu, Mtoni, Pukuchani ruins, hizi tutaziboresha ili mtalii akija kwa siku zake nane hawezi kuchoka.

**Swali: Kuna fursa ilitolewa kwa Zanzibar na Rais John Magufuli wiki iliyopita kwamba iuziwe wanyamapori kutoka hifadhi ya taifa. Hatua zipi zilizofikiwa hadi sasa?**

**Jibu:** Hiyo ofa tuliisikia na tulifurahi sana, kwa sababu katika plan zetu (mipango) tulisema tujenge national park, kwa sababu Zanzibar tuna sehemu za kihistoria, tuna beach (fukwe), lakini tuna miradi mingi ya kuanzisha ya kuibua vivutio vipya sehemu za kitalii. Focus yetu kwa sasa ni private enterprises kuhamasisha wawekezaji kuja kuwekeza katika shughuli za utalii na iwe rahisi kushindana. Serikali iwezeshe kuboresha miumbombinu, kama barabara, viwanja vya ndege, hilo tumelichukua na tunalifanyia kazi, kuna walioonyesha kuvutiwa na kuja kuomba katika miradi mbalimbali ya uwekezaji.

**Swali: Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), imeeleza kuwa ifikapo 2025 Tanzania iwe inapokea watalii kutoka milioni 1.5 hadi milioni sita, mapato ya utalii kutoka Dola za Marekani milioni 2.6 hadi Dola milioni sita. Je, Zanzibar imejipangaje?**

**Jibu:** Katika kipindi cha miaka mitano matarajio yetu kama tulivyoahidi kwenye ahadi zetu ni kuingiza watalii 800,000 na kutoa ajira 300,000 kwa upande wa Zanzibar. Wizara kwa upande wake itahakikisha inaongeza vivutio vya utalii pamoja na miundombinu ya hoteli. Vitu hivi vinapoongezwa namba ya ajira itaongezeka katika taasisi hiyo.

Mkakati wetu unasema Tourism for all (utalii kwa wote), kwa kuanzisha kamati za wilaya za utalii ambazo zitaongozwa na wakuu wa wilaya kuhamasisha wanavijiji husika kuangalia usalama wa watalii, shughuli za maendeleo za miradi ya utalii na kupewa nafasi za ajira katika vituo hivyo vya utalii. Hii inakuwa rahisi kwa kuwa mpaka mtu wa chini atafaidika katika eneo husika na kuchangia. Tumeamua kuwa watu wa chini kwa mfano walinzi, watoke eneo lile lile badala ya kutoka nje kwa sababu wanajisikia na wao sehemu ya mradi badala ya kuwa wapenzi watazamaji, hiki kitu katika sekta ya utalii hatutaki, tunataka kila mtu anufaike katika sekta hii.

**Swali: Mji Mkongwe ni sehemu ya kihistoria ya Zanzibar na hali ya majengo yake inaonyesha kuchoka. Je, serikali ina utaratibu gani wa kushirikisha wadau wengine ili kuyafanyia ukarabati na kurudisha hadhi yake?**

**Jibu:** Baada ya kuanguka Jumba la Maajabu, Rais Dk. Hussein Mwinyi, aliitisha kikao cha wizara pamoja na wadau wa mji mkongwe. Majengo yale yapo tangu mwaka 1800 na yamejengwa na mawe, udongo na chokaa, lakini mji wa stone town ni urithi wa dunia ambao Shirika la Umoja wa Mataifa UNESCO, linakuwa na masharti yake katika kuyajenga.

Katika huu ushirikiano na sekta binafsi tunafanya tathimini ya majengo yote kuhakiki kujua ubora wa majengo hayo, kuna mengine yapo katika hali mbaya ambayo watu wanatakiwa kuondoka na mengine ni ya kuboresha, ndiyo maana ya kuwashirikisha wadau, kwa sababu serikali haiwezi kumiliki kila kitu. Na katika yale majengo kuna yanayomilikiwa na serikali na mengine ya watu binafsi, cha msingi ni kuwasimamia katika kuboresha kwa kiwango ambacho UNESCO inataka. Kuna majengo ambayo ni mali ya Shirika la Nyumba Zanzibar na mengine ni kwaajili ya wakfu ambayo yapo kwaajili ya wakfu tangu kipindi hicho, kuna yale ambayo watu hawawezi kuishi tumeona tuyafunge kwanza yaweze kurekebishwa na ambayo hayafai ni bora watu kuwaondoa. Pia tumeona umuhimu wa kuanzisha mfuko wa mji mkongwe na serikali iko katika mchakato wa kuwezesha wadau kulipwa fidia na kutakuwa na fedha maalumu kwa ajili ya ukarabati.

**Swali: Jumba la Maajabu baada ya kuanguka litarudi katika hadhi yake ya zamani au litabadilishwa.**

**Jibu:** Jengo lilifanyiwa assessment na jana tumewapokea watu wa UNESCO kwa ajili ya kuliscan na umadhubuti wake, na kama litawezekana vipi liwe, lakini no matter what, lazima lirudi kama lilivyo. Jengo limeanguka likiwa katika mikono ya makandarasi. Kilichoanguka ni kuta na madirisha, ndani kulikuwa hakuna kitu chochote, vitu vyote vya kumbukumbu vimehifadhiwa. Jengo limeanguka asilimia 16.6 tu. Jengo lina muumiza kila Mzanzibari hatuwezi kukubali alama yetu kuondoka kirahisi.

Wafadhili Serikali ya Oman wamekuwa nasi bega kwa bega katika ujenzi, serikali tunachofanya ni kulilinda ili lisiendelee kuanguka kwa kuweka nguzo kufunika mabati ili ikitokea mvua lisiendelee kuharibika. Kwa hiyo msijali lile litarudi.

**Swali: Serikali ina mpango gani wa kurahisisha upatikani wa vipimo vya corona.**

**Jibu:** Zanzibar tunakusanya sample (sampuli) na kupima, inapotokea baadhi ya wakati pengine vifaa vinashindwa kufanyakazi ndiyo tunakwenda bara, lakini ni kweli kuna changamoto kupatikana kwa majibu inapotokea wageni kuwa wengi. Tumeweka vituo kama hospitali binafsi, kwa mfano Lumumba, Nungwe, vipimo vyote vinapimwa sehemu moja. Kama serikali tunahakikisha kero zote hizi zinapungua. Sampuli kwa wageni iko katika kituo cha Migombani. Lakini pamoja na changamoto hiyo tumesikia hata watu wa bara wanakuja Zanzibar kuchukua vipimo. Kila siku serikali iko katika kuboresha mazingira na sasa hivi sisikii tena malalamiko ya kuchelewesha kupata majibu.

Swali: Serikali imejipanga vipi kutumia mitandao ya kijamii kutangaza sekta ya utalii.

Jibu: Utalii ni biashara na biashara ni kujitangaza. Ndiyo changamoto kubwa tunaikuta sasa hivi, kwa sababu watu walikuwa wanasubiri watalii waje ofisini kuulizia. Kama serikali tunataka kutumia effectively mitandao ya kijamii. Tuna timu kama Yanga na Simba na watu mashughuli kutoa hamasa kwa kutumia kurasa zao kutangaza vivutio vyetu vya utalii katika mitandao ya kijamii.

HABARI KITAIFA

# Askari SUMA-JKT awekwa matatani

**Na Elizabeth Zaya**

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeelekeza kurudishwa Makao Makuu ya Kanda ya Jeshi hilo, Askari wa Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA-JKT), na kuchukuliwa hatua kulingana na taratibu za jeshi hilo.

Askari huyo anadaiwa kumpiga ndugu wa mgonjwa aliyekuwa amefika katika hospitali ya rufani mkoani Shinyanga Januari 22, mwaka huu.

Taarifa ya kurejeshwa kwa askari huyo ilitolewa jana na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Profesa Mabula Mchembe.

"Tumeelekeza mlinzi huyo atolewe kwenye kituo hicho cha kazi na kurudishwa Makao Makuu ya Kanda ya Jeshi hilo kwa ajili ya hatua za kinidhamu kulingana na taratibu za Jeshi hilo,"alisema Prof. Mchembe.

Prof. Mchembe aliagiza ufanyike uchunguzi kubaini endapo kulikuwa na uzembe wa utekelezaji wa mfumo na mwongozo wa utoaji huduma ambao ulitolewa na wizara hiyo katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya ili kubaini kama kulifanyika udhaifu na kushindwa kuzuia tukio hilo.

"Na baada ya uchunguzi huo hatua stahiki zitachukuliwa kulingana na yatakayobainika.,"alisema Profesa Mchembe.

"Tunawaomba wananchi wawe watulivu wakati suala hili linafanyiwa kazi, na jamii iendelee kupata huduma katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya bila wasiwasi wowote, kwani serikali imejipanga kuhakikisha suala hilo halijirudii."

Pia, aliwaomba wananchi kutumia vizuri mifumo ambayo imewekwa sehemu mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na simu zisizo za kulipia (199) kuwasilisha malalamiko ili kufikia maamuzi sahihi ya migogoro badala ya mapigano.

Aliwaomba wananchi kufuata na kuzingatia taratibu zilizowekwa ikiwamo muda wa kuingia na kutoka kuona wagonjwa katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini.

Prof. Mchembe aliwataka viongozi na watumishi wote kusimamia vizuri huduma bora kwa wateja ili kuondoa mitafaruku na migongano inayozuilika.

"Waganga wafawidhi wote wa Hospitali na Zahanati zote nchini wanakumbushwa kusimamia vizuri miongozo ya huduma kwa wateja ambayo ilishatolewa na Wizara ili kuwa na mazingira rafiki kati ya walinzi, watumishi na wagonjwa,"alisema Prof. Mchembe.

# Samia azitaka mahakama kutoa haki

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amezitaka mahakama kuhakikisha zinatoa haki kwa wastahili kwa kuzingatia mfumo wa sheria.

Amewasisitisha majaji, mahakimu na watendaji wengine wa muhimili huo wanatoa maamuzi bila vishawishi vya rushwa.

Pia, ameitaka Mahakama Kuu kuhakikisha inaharakisha mchakato wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ngazi zote za mahakama ili kuwasaidia wananchi wanyonge kupata haki zao za msingi pasipo kikwazo cha lugha.

Alitoa rai hiyo jana jijini Dodoma wakati wa maadhimisho ya Wiki ya sheria na miaka 100 ya Mahakama Kuu, na kueleza kuwa majaji wanapokuwa katika viti vyao wanatakiwa kuwa na nafsi safi, ambazo zitawasaidia kutoka haki kwa wanaostahili na badala ya kutoa haki kwa wasiostahili kwa kigezo cha rushwa.

Alisema haki ni msingi mkuu katika kuimarisha ustawi wa jamii, na kama itakiukwa itasababisha migogoro pamoja na kutoweka kwa amani.

Akizungumzia kuhusu umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika muhimili huo, Makamu wa Rais alisema wakati umefika lugha hiyo kutumika kwa ngazi zote za mahakama.

Alisema wananchi wamekuwa wakinyimwa haki zao za msingi kutokana na kikwazo cha lugha inayotumika katika mahakama.

"Ni aibu kwa miaka 100, ya Mahakama Kuu na taifa hili ambalo ni huru mwananchi wake anakosa haki yake kutokana na kigezo cha kutokujua lugha ya Kingereza, hivyo basi mchakato wa lugha ya Kiswahili unatakiwa ufanywe haraka ili kuwasaidia wananchi," alisema.

Pia, alisema wananchi wengi wa vijijini, bado wanatatizwa na kutofahamu vizuri taratibu mbalimbali za kufungua mashauri, uendeshaji wa mashauri na rufani.

Kadhalika, alitoa wito kwa taasisi zinazohusika na kukamata wahalifu, kufanya upelelezi na kuendesha mashauri ya jinai mahakamani kujikita katika mazingira ya vijijini ambako kesi nyingi hazifiki kwenye vyombo vya sheria au zinaishia njiani.

"Mnaweza kuangalia uwezekano kushirikiana na redio jamii katika maeneo husika kutoa vipindi mbalimbali ili kuelimisha umma. Vile vile kutumia umbe mfupi wa simu kuelimisha kuhusu sheria mbalimbali," alisisitiza.

Naye, Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Jum, alikiri kuwa lugha inayotumika mahakamani inaweza kuwa kikwazo katika kufikia dhana ya upatikanaji wa haki.

"Umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika shughuli za utoaji haki zimezungumzwa sana hivi karibuni. Tumezungumza pia na Mheshimiwa Dk. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu umuhimu wa lugha ya Kiswahili mahakamani,"alisema Prof. Juma.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Nadhifa Kemikimba na Mkurugenzi wa Shirika la Water Mission Tanzania, Benjamin Filskov, wakikata utepe kuzindua mradi mpya wa maji wa Ikombo uliopo Wilaya ya Chamwino, Dodoma.Mradi huo utahudumia wananchi wapatao 4,172 pamoja na taasisi za kijamii kama shule, kliniki pamoja na masoko. **PICHA: MPIGAPICHA WETU** .

# Agizo mikoa, wilaya usimamizi mwongozo biashara ya mazao

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

VIONGOZI wa mikoa na wilaya wametakiwa kusimamia mwongozo wa biashara wa mazao yanayotumia mfumo wa stakabadhi ghalani kwa mwaka 2021, ili kusaidia mkulima kutoingia kwenye mikono ya madalali wa mazao yao.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini, Dk. Benson Ndiege, alitoa maelekezo hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mwongozo wa mfumo wa mazao ya stakabadhi za ghalani wa mwaka 2021.

"Ninawaomba viongozi wote katika ngazi za mikoa na wilaya ambapo mazao yanayotumia mfumo wa ununuzi wa stakabadhi ghalani kusimamia utekelezaji wa mwongozo huu ili kuwasaidia wakulima wetu," alisema.

Aliyataja mazao mapya yaliyoingizwa kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani ni choroko, soya, ufuta, mbaazi na dengu.

Alisema mazao hayo yameingizwa kwenye mwongozo huo ambao utawataka wananchi wote kutumia ushirika katika kuuza mazao hayo.

Alibainisha kuwa mwongozo huo unatoa maelekezo kuwa mazao hayo yatakusanywa kwenye ghala za vyama za ushirika na kusafirishwa kwenda kwenye ghala kuu za minada ya kuuza mazao.

Kadhalika, alisema katika kutekeleza azma hiyo ya Serikali, Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) kwa kushirikiana na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) wameandaa mwongozo huo wa biashara wa 2021.

Dk Ndiege alisema taarifa za mazao yaliyopokelewa ghala kuu zitatumwa soko la bidhaa na kuuzwa kwa minada kwa njia ya kieletroniki .

Aliongeza kuwa mfumo huo utawasaidia wakulima wadogo na wakubwa kuingia kwenye mfumo wa kujadili bei ya mazao kwa pamoja na kuwa na uwazi katika soko kwa wanunuzi.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Taifa Stars itavuka CHAN ikiiva Guinea kama fainali*

**TIMU** ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, keshokutwa, Jumatano itashuka tena dimbani nchini Cameron kwenye mechi yake ya mwisho ya Kundi D ya Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) baada ya Jumamosi kuibuka na ushindi wake wa kwanza katika michuano hiyo kwa kuifunga Namibia bao 1-0.

Stars, ambayo ilianza kwa kupoteza kwa mabao 2-0 dhidi ya Zambia, Jumatano itavaana na Guinea iliyopo kileleni mwa Kundi D ikiwa na pointi nne sawa na Zambia inayoshika nafasi ya pili kutokana na kuzidiwa kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Hata hivyo, ushindi pekee ndio utakaoiwezesha Taifa Stars yenye pointi tatu katika nafasi ya tatu, kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo inayoshirikisha jumla ya timu 16 zikiwa zimepangwa katika makundi manne kila moja likiwa na timu nne.

Katika Kundi D, Namibia ndiyo inaburuza mkia kutokana na kupoteza mechi zake mbili na siku hiyo ya Jumatano itakuwa ikicheza dhidi ya Zambia ambayo itakuwa ikihitaji sare yoyote ili kusonga mbele kama ilivyo kwa Guinea.

Kwa ujumla katika kundi hilo, mchezo kati ya Guinea na Stars, ndio utakaokuwa mgumu zaidi kwani Tanzania itakuwa ikihitaji ushindi ili kusonga mbele huku wapinzani wao, sare yoyote ikiwapa tiketi ya kutinga robo fainali.

Tunaamini hakuna njia ya mkatao ya kuweza kupata matokeo zaidi ya wachezaji kujituma mwanzo mwisho na kuuchukulia kama fainali mchezo huo utakaopigwa majira ya saa 4:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki.

Lakini pia tunaamini Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije pamoja na wasaidizi wake, Suleimani Matola na Juma Mgunda, tayari wanafahamu ubora, uimara na udhaifu wa Guinea, hivyo watakuwa wamewapa mbinu zaidi wachezaji wao ili kuibuka na ushindi na kisha kutinga robo fainali ya michuano hiyo kwa mara ya kwanza baada ya mwaka 2009 kuishia hatua ya makundi.

Pamoja na kwamba utakuwa mchezo mgumu kwa Stars kutokana na ubora wa Guinea, ni wakati wa kila mchezaji kutambua na kuona thamani ya kuthaminiwa na Watanzania zaidi ya milioni 50 kwa kupewa dhamana ya kuvaa jezi ya taifa na kwenda kuipeperusha bendera ya nchi katika mashindano hayo ya pili kwa ukubwa barani Afrika kwa ngazi ya timu za taifa.

Hata hivyo, kutokana na ubora wa timu ya Guinea na mchezaji mmoja mmoja, njia pekee ya Stars kuibuka na ushindi, ni kucheza kitimu zaidi na kutokata tamaa mwanzo mwisho kila mmoja akitambua hiyo ni nafasi pekee kwake ya kuonyesha kocha hakukosea kumjumuisha katika kikosi hicho.


Tunalazimika kuyasema hayo kutokana na kutambua wapo mashabiki wengi na wadau wa soka nchini, ambao wanakibeza kikosi cha Stars kutokana na kuonyesha kiwango cha chini katika michuano hiyo, lakini pia tangu mwanzo wakionyesha kutokukubaliana na uteuzi wa wachezaji uliofanywa na Ndayiragije kuunda kikosi hicho.

Hivyo, njia pekee ya kuwafunga mdomo wote wanaowakosoa na wasiowakubali, ni wachezaji kuonyesha ubora na kujituma zaidi katika mechi hiyo ya mwisho ili kushinda na kutinga hatua ya robo fainali.

Nipashe tunaungana na Watanzania wote wanaoitakia kila la kheri Taifa Stars kupata ushindi kuelekea mechi hiyo ya Jumatano, lakini pia tukiendelea kuwasisitiza wachezaji wasituangushe kwani tunachotaka ni ushindi tu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

## *Taifa Stars moja, makocha milioni moja!*

**AFADHALI** sasa Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije, atapumua na kupumzika kutoka kwenye midomo ya baadhi ya watu ambao walikuwa wanataka atimuliwe.

Hii ni baada ya timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, kufungwa mabao 2-0 dhidi ya Zambia kwenye mechi ya kwanza ya Kundi D, ya Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zinazoendelea nchini Cameroon.

Ushindi wa bao 1-0 ilioupata dhidi ya Namibia Jumamosi usiku, umeifanya timu hiyo si tu kujizolea pointi tatu na kuweka hai matumaini ya kutinga hatua ya robo fainali, lakini yamewafanya wale wote ambao walikuwa wameshaanza kumnyooshea kidole cha shahada kocha huyo, sasa kunyamaza. Baada ya kipigo, baadhi ya mashabiki, waandishi wa habari za michezo, na wachambuzi, walishaanza kusema kuwa kocha huyo hafai.

Ni kocha huyu huyu ambaye ndiye ameipeleka Stars kwenye fainali za CHAN ndiye leo anaambiwa hafai. Na ukisikiliza sababu unaambiwa kuwa hakuchagua kikosi kizuri cha kwenda nacho CHAN. Wengine wanasema ana kikosi kizuri, lakini anakosea kukipanga na wapo ambao hawana hata sababu, wao wanasema tu hafai.

Kuna mashabiki wako tofauti na Ndayiragije kwa sababu tu hakuwachagua baadhi ya wachezaji ambao wao wanaona wanafaa kuichezea timu ya taifa. Hili ndilo tatizo la baadhi ya mashabiki wa soka Tanzania na wachambuzi wa masuala ya michezo.

Taifa Stars inapofungwa mara nyingi hazitolewi sababu za kitaalam, au za msingi kabisa za soka letu, badala yake zinakuwa ni za kishabiki na kisiasa zaidi. Wakati mwingine Stars inaweza kufungwa tu kwa sababu imezidiwa kwa kukutana na timu bora au kwa siku hiyo imekuwa bora kuliko Stars, lakini watu hawataki kukubali ukweli huo.

Sidhani kama leo Watanzania tumekuwa na timu imara ambayo haitakiwi kufungwa kwenye michuano yoyote ile.

Na hata kama Stars ikishinda, basi si kwamba tuna timu imara sana, ila wakati mwingine mbinu za benchi la ufundi kwa siku hiyo zimefanya kazi nzuri, au tumekutana na timu ambayo tumeizidi kiwango kwa siku hiyo.

Hakuna sababu yoyote ya Stars kufungwa basi tatizo liwe kwa kocha Ndayiragije. Stars imefundishwa na makocha wengi sana na wameondoka, lakini bado matatizo ni yale yale. Hakuna kocha yeyote atakayekuja na kuleta miujiza kama Stars itakuwa na aina ya wachezaji wale wale ambao leo wanacheza vema, lakini kesho wanacheza vibaya.

Mashabiki wengi wa Tanzania wanakwepa sababu za msingi kuwa wachezaji wetu hawajaandaliwa kuwa wanasoka, hasa wa kulipwa, ndiyo maana mchezaji wa Ligi Kuu wakati mwingine hata kutuliza mpira anashindwa, lakini pia baadhi wanashindwa hata kulinda viwango vyao.

Mara nyingi sababu za Watanzania utasikia kocha mbaya, kocha anabagua wachezaji, hawezi kupanga kikosi, hajaita wachezaji fulani. Na wengine wanakwenda mbali kabisa na kusema ili Tanzania iwe na timu nzuri ya taifa ni lazima wapunguzwe wachezaji wa kigeni nchini.

Hata hivyo, ukiangalia mechi zote mbili za Stars, utaona kwa kiasi kikubwa wachezaji wa Kitanzania wameshaondoa hofu ya kucheza na wachezaji wageni kwa sababu kwenye ligi yao kuna wachezaji wengi kutoka mataifa tofauti.

Kwa maana hiyo, kuwapo kwa wachezaji wa kigeni kwenye ligi yetu, kunawafanya wachezaji wetu sasa wacheze kwa kujiamini.

Tatizo ni moja tu, wakati mwingine wanazidiwa uwezo tu wa mchezaji mmoja mmoja na wachezaji wa timu zingine. Inawezekana wakosoaji wakaibuka tena Jumatano kwenye mechi dhidi ya Guinea, ingawa hatuombei hilo litokee.

Hapa nataka kusema mambo ya ufundi tumuachie kocha mwenyewe. Stars ina kocha mmoja tu ambaye ni Ndayiragije, wengine wote tubaki kuwa washangiliaji na timu ikipata matokeo ya aina yoyote tuwe tumefungwa wote na si kumtupia lawama kocha, kwa sababu wachezaji Stars ni hawa hawa, hakuna wengine wenye viwango vya juu zaidi hapa Tanzania kuliko hawa waliokuwapo.

# Wananchi, mbunge kujenga kituo cha polisi

**Na Dinna Maningo,** TARIME

WANANCHI wa kata ya Itiryo, wilayani Tarime mkoani Mara kwa kushirikiana na Mbunge wa Jimbo la Tarime vijijini, Mwita Waitara, wamechanga fedha ili kujenga kituo cha polisi kwa lengo la kuimarisha ulinzi na kupambana na uhalifu.

Baadhi ya matukio ya uhalifu yamedaiwa kufanywa na watu wa nchi jirani kwa kushirikiana na baadhi ya Watanzania wanaoishi mpakani.

Waitara akizungumzia suala la ulinzi na usalama katika maeneo ya mipakani, alisema anachukizwa na vitendo vya mauaji na uhalifu vikiwamo vya watumishi wa serikali kuvamiwa na kuporwa fedha na mali.

"Tukio la mwalimu kuuawa liliteta taswira mbaya na nilitumia nguvu nyingi kulishughulikia, lakini bado watu hawasikii wanaendelea na vitendo vya uhalifu na kuchukua mali za watu, kuna mwananchi wa kijiji cha Itiryo alipigwa risasi akafa, na inaelezwa kuwa majambazi wanatoka nchi jirani ya Kenya na wanashirikiana na wahalifu kutoka kata ya Itiryo," alisema Waitara.

Waitara alisema matukio ya kihalifu yamezidi kuleta hofu kwa watumishi wa serikali wakiwamo walimu wa shule ya msingi kata ya Itiryo huku baadhi yao wakiomba uhamisho ili kunusuru maisha yao jambo ambalo linaweza kurudisha nyuma taaluma ya wanafunzi.

"Nimeambiwa kuwa kuna walimu wanataka kuhama matukio kama haya yanashusha heshima ya kabila letu la Wakurya na ndiyo maana tunachukuliwa kama ni watu wakorofi, kwanini tuwafiche wahalifu, lazima tuwataje kwa njia zozote hata kama ni kwa siri ili wakamatwe tukiyaacha haya maovu watu watahama kata na uchumi utashuka, kwa kuwa mmekubali kituo kijengwe nachangia milioni tano ya ujenzi, " alisema Waitara.

Nchagwa Matare, alisema suala la kujengwa kituo cha polisi lilishazungumzwa na kuna maeneo ambayo yanaweza kutumika kukijenga na kuwaomba viongozi wa serikali za vijiji kuhamasisha wananchi kuchangia fedha na nguvu kazi.

# Wanaowatoza wawekezaji gharama za ziada kukiona

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewataka wawekezaji wa nje na ndani wasisite kuwekeza nchini.

Pia amewataka kutosita kutoa taarifa serikalini pale watakapotozwa gharama za ziada.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa mwongozo wa uwekezaji mkoa wa Iringa na amesema kwamba Serikali itaendelea kudumisha amani na utulivu ambao ni muhimu kwa wawekezaji na wananchi.

Alisema uwekezaji ni tegemeo la Taifa katika kukuza uchumi wake na kuongeza ajira, hivyo serikali inaendelea kuimarisha usimamizi wa watumishi wa umma wanaohusika na utoaji wa huduma kwa wawekezaji kwa lengo la kuhakikisha kuwa hawasumbuliwi, na pale ambapo hawatohudumiwa vizuri ikiwamo kutozwa gharama za ziada watoe taarifa kwa mamlaka husika.

Akizindua mwongozo huo katika Chuo Kikuu cha Mkwawa, alisema umebainisha vivutio vilivyoko mkoani Iringa ikiwamo mazingira mazuri ya biashara, nguvu kazi, amani na utulivu, maliasili nyingi na soko la kutosha.

"Iringa umejaliwa kuwa na fursa nyingi za uwekezaji. Hata hivyo, kuwa na fursa ni jambo jema, lakini kuwapata wawekezaji makini ni jambo la muhimu zaidi. Wadau hususan wafanyabiashara wanapaswa kuzifahamu fursa hizi kwa kina ili waweze kuja kuwekeza.

"Mkoa uendelee kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo sambamba na kuondoa vikwazo vyote vya uwekezaji na biashara ili kuvutia zaidi wawekezaji wa ndani na nje."

Alisema dhamira ya Serikali ni kuongeza kasi ya uwekezaji katika sekta zote, na kwamba wawekezaji wakija wawe kama marafiki na wadau muhimu kwa maendeleo ya Taifa na waungwe mkono kwenye maeneo watakayohitaji kuwekeza.

"Tuondoe vikwazo visivyo vya lazima na iwapo wamefuata taratibu zinazopaswa, sitegemei kuona wawekezaji wakikwamishwa kutekeleza miradi yao katika kila sekta na kila mkoa."

Waziri Mkuu alisema katika kutimiza azma hiyo, watendaji wote wa Serikali katika ngazi mbalimbali wanapaswa kushiriki kutangaza fursa hizo za uwekezaji na pia kutatua changamoto mbalimbali zilizopo katika sekta wanazozisimamia ili kurahisisha mazingira ya biashara na uwekezaji katika maeneo mbalimbali.

"Katika ziara zangu za mikoani nimesisitiza sana umuhimu wa watumishi wa umma kuwatumikia wananchi wote kwa usawa na bila ubaguzi. Aidha, nimeagiza wananchi wote na wageni wakiwamo wawekezaji wanapofika kwenye Ofisi zote za umma, wapokelewe kwa staha, wasikilizwe na kupewa huduma wanazohitaji kwa uharaka na ufanisi bila urasimu."

Alisema katika kipindi cha miaka mitano, wananchi wameshuhudia jitihada kubwa na za wazi zilizofanywa na Serikali katika kutoa msukumo wa maendeleo katika nyanja mbalimbali zikiwamo za kiuchumi na kijamii na viashiria vingi vya kiuchumi na kijamii vimeonyesha matokeo mazuri.




Watoto, ndugu jamaa na marafiki wakiweka mashada ya maua kwenye kaburi la Hayati Mchungaji Getrude Rwakatare lililopo kwenye Kanisa la Mlima wa Moto Mikocheni jijini Dar es Salaam, walipokwenda kanisani kutoa shukrani kwa shule za St Mary's kuendelea kufanya vizuri kitaaluma mwaka mmoja baada ya kifo cha mwanzilishi wake. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE** .

# Mradi kunufaisha wakulina wa mtama

**Na Mwandishi Wetu**

Kampuni ya Bia (TBL) imeongeza ushirikiano na Shirika la Mpango wa Chakula (WFP) katika mradi wa pamoja wa kuendeleza zao la mtama msimu wa mwaka 2021.

Mradi utashirikisha wakulima 4,000 ambao wanatarajiwa kuzalisha tani 10 za mtama.TBL imekubali kununua mtama huo kwa bei ya Sh. 550 kwa kilo.

Mkurugenzi Mtendaji wa TBL Plc, Philip Redman, alisema mradi wa mwaka 2021 ni mwendelezo wa mradi wa pamoja wa majaribio uliopata mafanikio makubwa kwa kuongeza mavuno kwa asilimia 70 zaidi ya mwaka uliotangulia.

Alisema pia mradi wa majaribio ulilenga kufanya kazi na wakulima 2,000 kwa kuwapatia elimu ya kilimo cha kisasa, namna ya kuboresha mavuno na ubora wa mtama sambamba na kuwapatia soko la uhakika la mazao watakayozalisha.

Wakulima watawezeshwa kupata mkopo kutoka benki ya NMB Bank na kukata bima kutoka kampuni ya Jubilee na kupatiwa mbegu bora kwa mkopo, mbolea na pembejeo wanazohitaji ambapo gharama hizo zitalipwa wakati wa kipindi cha mwisho cha msimu wa mavuno.

Uzinduzi wa usambazaji wa mbegu za mtama ulifanyika wilayani Kongwa hivi karibuni ambapo maofisa kilimo kutoka TBL walifanya mikutano na wakulima kujadili changamoto wanazokabiliana nazo na kukutana na mawakala wa huduma ya bima ili kuwapatia wakulima elimu ya bima.

Meneja Kilimo wa TBL Plc, Joel Msechu alisema: "Msimu huu kampuni imezindua teknolojia ya BanQu ambayo itawanufaisha wakulima 4,000 kwa kuwa inaongeza uwazi na ufuatiliaji katika katika mnyororo wao wa ugavi.

Mmoja wa wakulima wa mtama ambaye pia ni Katibu wa Kikundi cha Wakulima wa mtama Kijiji cha Sagara B, wilayani Kongwa, Theodora Mgaya, akizungumza kwa niaba ya wenzake wakati wa mafunzo ya matumizi ya teknolojia ya BanQu yaliyofanyika mwishoni mwa wiki, aliishukuru TBL na washirika wake kwa kuwajengea uwezo kupitia kilimo cha mtama ambacho hapo awali kilikuwa sio cha kibiashara.

# Serikali yakabidhi hifadhi kwa TAWA

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

HATIMAYE Serikali imekabidhi usimamizi wa eneo la Hifadhi ya Wanyamapori ya Isawima wilayani Kaliua kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) ili kukomesha uharibifu maliasili ikiwemo ukataji magogo na uwindaji haramu wa wanyamapori unaofanyika katika eneo hilo.

Hatua hiyo inafuatia Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Isawima kushindwa kudhibiti vitendo vya uharibifu na mauaji ambayo yanaendelea katika hifadhi hiyo.

Makabidhiano ya awali yalifanywa jana na Mkuu wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, kwa niaba ya Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, kwa kuipa TAWA ili kuanza kazi ya kulinda hifadhi hiyo.

Alisema Serikali imechukua hatua hiyo baada ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Isawima kutokamilisha taratibu za usajili na kutokuwa na uwezo na nguvu za kisheria za kuisimamia hifadhi hiyo, hali iliyopelekea kuendelea kwa ujangili, mauaji na kusababisha tishio kubwa la kutowekwa kwa hifadhi hiyo.

Dk. Sengati alisema Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Isawima haina rasilimali za kutosha kukabiliana na uharibifu katika eneo hilo na hivyo kufanya kuwepo kwa makundi ya wavamizi ndani ya mistu.

Alisema kufuataia kukosekana kwa rasilimali vitu na watu wamekuwa wakingoja uharibifu utokee ndio waende kwa ajili ya kujipatia fedha toka kwa waharifu zinazotokana na uuzaji wa magogo na faini, badala ya kufanya kazi ya kuzuia uharibifu kwa ajili ya uendelevu wa maliasili hiyo muhimu kwa maendeleo ya Taifa.

Dk. Sengati alisema mtindo huo wa usimamizi umesababisha kuzuka kwa migogoro ya mara kwa mara ambayo kwa upande mwingine imesababisha hata watu kupoteza maisha.

Aliitaka TAWA baada ya kupewa jukumu hilo kufanyakazi kwa uzalendo katika kulinda rasilimali hiyo muhimu kwa wakazi wa mikoa ya Tabora na Kigoma ili Serikali isije ikaona kuwa imekosea kuwapa jukumu la usimamizi.

Dk. Sengati aliongeza kuwa katika usimamizi ni vema wakaendelea kushirikiana na vijiji vilivyotoa ardhi yao kwa ajili ya uanzishaji wa hifadhi hiyo ili nao waone manufaa ya kuwepo kwake.

Alisema wanaweza kuwashirikisha kwa kuwaruhusu kufanya shughuli ambazo haziathiri uhifadhi kama vile ufugaji wa nyuki katika eneo la Hifadhi na kutoa michango kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo kama kuwajengea shule na zahanati sehemu ambazo hawana.

Aliwataka kuhakikisha wavamizi wote na vikundi vyote vya uhalifu vilivyomo ndani ya msitu huo vinaondoka ili uharibifu usiendelee.




Makamu wa Rais, Samia Hassan (kulia), akipita mbele ya banda la maonesho la Benki ya NMB, alipokuwa akikagua mabanda ya kwenye maonesho ya Wiki ya Sheria mwaka 2021 na maadhimisho ya Miaka 100 ya Mahakama Kuu ya Tanzania katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma jana. Makamu wa Rais alifungua rasmi maonyesho na NMB ni miongoni mwa benki washiriki wa maonyesho hayo kitaifa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kibiti yapigwa jeki madawati 100

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI ya vinywaji ya Coca-Cola Kwanza imekabidhi madawati 100 ya thamani ya Sh. milioni 10 kwa uongozi wa Wilaya ya Kibiti mkoani Pwani.

Akizungumza wakati wa kukabidhi madawati hayo, Mkurugenzi anayeshughulikia masuala ya Umma, Mawasiliano na ukuaji endelevu wa kampuni hiyo, Salum Nassor, alisema lengo ni kuunga mkono jitihada za serikali katika kuinua sekta ya elimu pamoja na kupunguza tatizo la ukosefu wa madawati hayo hususani katika kipindi hiki cha mwanzo wa mwaka ambacho wanafunzi wengi wanajiunga na masomo.

Alisema ipo haja ya kila mdau kuunga mkono jitihada za serikali za kuinua sekta hiyo hususani katika kipindi hiki cha elimu bure.

Alisema Coca-Cola Kwanza itaendelea kuhakikisha kwamba maisha ya Watanzania yanastawi kwa kuendelea kuunga mkono juhudi hizo za maendeleo katika jamii na nchi kwa ujumla.

"Kampuni yetu imejipanga kusaidia maendeleo ya Watanzania katika nyanja mbalimbali, lengo letu kama kampuni ni kurudisha shukrani kwenye jamii kwa sababu imekuwa ikishirikiana na sisi kwenye kuchochea shughuli za maendeleo ya kijamii na ya kiuchumi katika taifa letu," alisema Nassor.

"Madawati haya tuliyotoa leo yametokana na mbao maalumu zinazotumiwa kubeba malighafi za utengenezaji wa vinywaji vya kampuni yetu, na hii ni dhana na dira ya Coca-Cola katika kurejeresha bidhaa zetu kwa ajili ya matumizi dhabiti ya rasilimali zetu na utunzaji wa mazingira."

Mkurugenzi huyo wa Coca-Cola Kwanza aliwakumbusha wadau, taasisi na Asasi zisizo za kiserikali kuungana na serikali katika kutafuta suluhisho na njia bora za kukabiliana na changamoto zinazoikumba jamii kwa njia ya ushirikiano kati ya taasisi hizo na serikali.

Mbunge wa Kibiti, Twaha Mpembenwe alisema msaada huo wa madawati umefika wakati muafaka wa kuanza muhula mpya wa masomo. Alisema kwa sasa shule zinapokea idadi kubwa ya wanafunzi kutokana na wazazi kushawishika kuwapeleka watoto wao shuleni kwa sababu ya elimu bila malipo na kwamba madawati hayo yanahitajika kwa wingi.

Nae mkuu wa Wilaya hiyo, Gullam Kifu, alipongeza sekta binafsi kwa kuendelea kushirikiana na serikali katika shughuli za maendeleo katika jamii.

# Shirika la ujenzi mradi wa maji lapongezwa

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Nadhifa Kemikimba, amelipongeza Shirika la Water Mission Tanzania kwa kufanikisha ujenzi wa mradi wa maji wa Ikombo, wilayani Chamwino, ambao utasaidia kutoa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi wapatao 4,172.

Mradi huo wenye thamani ya Sh. milioni 300, uliojengwa kwa ushirikiano kati ya Shirika hilo, Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) na wananchi utasaidia kupunguza adha ya maji kwa zaidi ya asilimia 97. Pia, utasaidia kutoa huduma kwenye kliniki, hospitali pamoja na shule kwenye eneo hilo.

Akizungumza hivi karibuni wakati wa uzinduzi wa mradi huo, Naibu Katibu Mkuu, ambaye alimwakilisha Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema mradi huo ni sehemu ya miradi mingi ya maji vijijini yenye lengo la kuhakikisha hadi ifikapo mwaka 2025 wananchi wanapata huduma ya maji kwa asilimia 95.

Alisema lengo la mradi huo ni kuwapatia wananchi wa Ikombo majisafi na salama karibu na makazi yao, ili kuwapunguzia adha na muda wa kutembea umbali mrefu badala ya kufanya shughuli zingine za maendeleo.

"Utaratibu ni kwamba kila baada ya mita 400 kuwe na bomba la majisafi na salama na ndani ya nusu saa mwananchi awe ameteka maji na kuondoka."

Kemikimba alilishukuru Shirika la Water Mission kwa msaada mkubwa walioutoa kugharamia mradi huo muhimu na kuahidi serikali na wananchi kuuendeleza.

"Nawashukuru Shirika la Water Mission kwa msaada mkubwa mlioutoa kugharamia mradi huu muhimu, naahidi serikali na wananchi tutaulinda ili udumu zaidi ya miaka mingi zaidi ili vizazi vilivyopo na vijavyo viweze kunufaika na mradi huu," alisema.

# TBS yatoa elimu bidhaa za vipodozi

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limeendelea kufanya ukaguzi na kutoa elimu kuhusu makundi 13 ya bidhaa za vipodozi kutokana na watu wengi kukumbana na tatizo la kutambua maana ya bidhaa hiyo.

Hatua hiyo ni sehemu ya mkakati wa Shirika hilo la kufanya ukaguzi unaoendana na kutoa elimu ya vipodozi kwa wananchi katika wilaya zote za mikoa ya Kanda ya Ziwa na tayari ukaguzi na elimu imetolewa kwenye Wilaya za Nyamagana na Ilemela, jijini Mwanza.

Akizungumza wakati wa ukaguzi wa bidhaa hizo uliofanywa na ofisi ya TBS Kanda ya Ziwa, Kaimu Mkuu wa kanda hiyo, Evarist Mrema, alisema ukaguzi huo ukiendana na kutoa elimu, unafanyika kwenye maduka ya rejareja, jumla, kwa wasambazaji, supermarkets, migahawa na kwingineko.

Akifafanua zaidi, Mrema alisema; " Tunafanya ukaguzi na kutoa elimu kwa upande wa vipodozi, kwani watu wamepata changamoto ya kujua ni nini maana ya bidhaa za vipodozi, tunaliona hilo nalo ni changamoto kwenye ukaguzi huu na tunahitajika kutoa elimu na tunatoa elimu na tunaendelea kutoa elimu wakati wa ukaguzi."

Alisema aina za vipodozi zipo katika makundi 13 na kundi la kwanza ni za bidhaa za watoto kama poda, shampuu na kundi la pili ni la bidhaa zinazotumika bafuni.

"Huko nako kuna bidhaa tofauti zinazotumika bafuni kama sabuni za kuogea pamoja na zile ambazo watu wanaziandaa katika maeneo yao ya kuogelea na vitu kama hivyo," alisema Mrema.

Alitaja kundi lingine kuwa ni bidhaa za nywele ambako kuna makundi yake kama mawili au matatu. Kwa mujibu wa Mrema kuna rangi za nywele ambazo zinatumika kwenye nywele, lakini pia kuna nywele zinazoongezwa ndani ya nywele asili kama rasta na wigi na kwamba hizo zote ni aina za bidhaa za vipodozi.

Bidhaa nyingine kwa mujibu wa Mrema ni ambazo zinapakwa juu ya ngozi kama mafuta ya kupaka, losheni na bidhaa nyingine zinazotumika kwa upande vidole vya kinamama mfano kucha bandia na rangi za midomo ambazo nazo ni sehemu ya bidhaa za vipodozi.

Alitaja aina nyingine za bidhaa za vipodozi kwa upande wa urembo zinazotumika kwenye macho kuwa zote hizo ni aina za vipodozi.

# Wasindikaji mpunga walilia soko la mchele

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WASINDIKAJI wa mchele wilayani Kahama, wameiomba serikali kuwatafutia soko la mchele la pamoja litakalosaidia kutoa bei elekezi yenye tija kwa wafanyabiashara nchini na wanunuzi wa bidhaa hiyo kutoka nchini za Afrika Mashariki na Kusini mwa Jangwa la Sahara (SADC).

Hayo yalibainishwa jana wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kuzalisha mchele bora wenye viwango vinavyokidhi ushindani katika soko la ndani na nje ya nchini, yaliyotolewa na Baraza la Mchele Tanzania (RCT), kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti (REPOA) kupitia mradi wa TradeCom II.

Victor Muzo, mfanyabiashara na msindikaji kutoka Shinyanga alisema, kila mmiliki wa mashine ya kusindika mchele ana bei yake ya kuuza hali inayosababisha wateja kutotambua bei sahihi ni ipi na kusababisha bidhaa hiyo kununuliwa kinyemela.

Alisema, ili kuwa na bei ya pamoja ni vyema serikali ikaunda ushirika kwa wasindikaji wa mchele kila wilaya zinazolima mpunga ili kuwa na bei moja kama ilivyo kwa wakulima wa zao la pamba na tumbaku pamoja na kusaidia kupata soko la uhakika kutoka nchi za SADC.

"Maisha yetu yameshikiliwa na madalali, wanaotupangia bei hasa tunapopata tenda kubwa, tunashindwa kukataa kwa sababu kila mashine inayosindika mchele ina bei yake, tunaomba serikali kutengeneza ushirika ili tuwe na bei moja na yenye tija," alisema Muzo.

Naye Haroun Msuya alisema, mchele umekuwa ukishuka bei kwa sababu ya ukosefu wa masoko ya uhakika ya ndani na nje, awali wateja wao wakubwa walikuwa wafanyabiashara kutoka nchini Rwanda, Kenya, Uganda na Kongo ambayo mipaka imefungwa na walizuiliwa kuja kununua.

Asha Hassani alidai, eneo walipojenga viwanda vya uchakati wa mchele liko mjini kati na halikidhi mahitaji na kuiomba serikali kuwatengea eneo lingine kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vikubwa na kuwatafutia mikopo yenye riba nafuu ili kuwekeza zaidi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa RCT, Winnie Bashagi alisema, zao hilo linalochangaia Pato la Taifa kwa asilimia 2.6, hulimwa katika wilaya 64 nchini na zaidi ya kaya asilimia 18 zinanufaika na zao hilo.

Akifungua mafunzo hayo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Timoth Ndanya, aliwataka wafanyabiashara na wasindikaji wa mchele kutumia kituo cha uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kusindika mchele katika hali ya ubora, usafi na kutambua soko liko wapi.

Pia, aliwataka kuwa na uhusiano mzuri na wakulima wa zao hilo sehemu zote zinazolima mpunga na kuacha kulima zao hilo kwa kutegemea mvua ambazo hupata mavuno ya wastani wa tani 3.5 kila mwaka huku wakitumia kilimo cha umwagiliaji kupata zaidi ya tani sita za mpunga.



Meneja Kilimo wa TBL Plc, Joel Msechu, akitoa mafunzo ya mfumo wa matumizi ya teknolojia ya BanQu kwa wakulima wa mtama wa Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma katika mafunzo yaliyofanyika wilayani humo mwishoni mwa wiki . **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Kilimo cha mboga na matunda chatajwa fursa

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WATANZANIA wameshauriwa kulima kilimo cha mboga na matunda kutokana na kuchukua muda mfupi kupata mavuno na kutoa faida kubwa kifedha.

Baadhi ya wakulima wa mboga mkoani Morogoro walisema hayo walipokuwa wanatoa maoni yao juu ya utafiti uliofanywa na Mtandao wa Wakulima Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESAFF), kama kuna athari zozote kwa wakulima uliporipotiwa Ugonjwa wa Covid 19 unaoeneza virus vya corona.

Wakulima wengi waliohojiwa walidai kutoathiriwa na ugonjwa huo, badala yake wale wanaolima mboga na matunda walivahimiza wananchi kugeukia kilimo hicho kwani mavuno yake hupatikana muda mfupi baada ya kupanda, na kwamba ni lishe muhimu kwa wagonjwa pamoja na kuwa na faida kubwa kifedha.

Landport, mjini Morogoro ambaye kwa takribani miaka mitano amekuwa akilima mchicha na tembele, alisema:

"Kilimo cha mboga kina unafuu mkubwa kiuwekezaji kutokana na gharama zake kuwa chini, mafanikio nayaona maradufu."

Akabainisha zamani alikuwa akijihusisha na ununuzi wa nafaka, lakini hakuwa akipata faida kama alivyotarajia, hivyo kuachana na biashara hiyo na kuamua kulima mboga.

Nao baadhi ya wafanyakazi ndogo katika mashamba ya mboga, Kibua Ali, Haruni Daudi na Ezekiel Kipande walisema shughuli hizo zimekuwa zikiwapatia uhakika wa kipato kila siku na kufanya familia zao kuwa na uhakika wa kuishi na kufanya shughuli zingine za maendeleo zikiwamo elimu, afya na mitaji ya biashara.

HABARI KITAIFA

## Kampeni tokomeza TB yazinduliwa Tunduru

**Na Neema Hussein,** RUVUMA

HOSPITALI ya Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, imezindua rasmi kampeni ya kutokomeza maambukizi ya ugonjwa wa kifua kikuu mwaka 2021 kwa kuanza kuwatumia wanachama wa Chama cha Msalaba Mwekundu (Red Cross), kama mkakati utakaowezesha kupunguza na kuwaibua watu wengi wanaougua ugonjwa huo.

Wanachama hao, wataungana na wataalam wa kitengo cha kifua kikuu na ukoma wa hospitali ya wilaya katika kutokomeza ugonjwa huo na kwa Mkoa wa Ruvuma wilaya hiyo inaongoza kwa maambukizi makubwa ya kifua kikuu.

Mratibu wa kifua kikuu na ukoma wa wilayani hapo, Dk. Mkasange Kihongole amesema, wameamua kuwatumia na kuwashirikisha wanachama wa Chama cha Msalaba Mwekundu kutokana na umuhimu wao katika jamii kwa kuwapa mafunzo yatakayowasaidia kushiriki vyema katika mapambano ya ugonjwa huo.

"Uzinduzi wa mapambano ya kifua kikuu katika wilaya yetu kwa mwaka 2021 tumeanza na wanachama wa Chama cha Msalaba Mwekundu kutokana na ukaribu wao na jamii, kwa hiyo tumelazimika kuwapa elimu kwa kuamini kuwa tutaongeza kasi ya kuwaibua wagonjwa wengi zaidi wa kifua kikuu katika wilaya yetu kama ilivyokuwa mwaka 2020," alisema.

Alisema, uzinduzi huo utafanyika na kampeni ya kuelimisha na kuchunguza vimelea vya ugonjwa huo katika maeneo mbalimbali ikiwamo taasisi za serikali, shule kwa shule, nyumba kwa nyumba na kwenye vilinge vya waganga wa tiba asili na tiba mbadala.

# KACU yatoa matofali 2,000 kukamilisha ujenzi madarasa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

CHAMA Kikuu cha Ushirika wilayani Kahama mkoani Shinyanga (KACU), kimetoa msaada wa matofali 2,000 katika Shule ya Msingi Nyahanga 'A' yenye thamani ya Sh. milioni 2.4 kwa ajili ya ukamilishaji na ujenzi wa vyumba vya madara ili wanafunzi wapate mahala safi na kusomea.

Shule hiyo iko Kata ya Nyahanga, Halmashauri ya Mji wa Kahama ikiwa na wanafunzi 1,335, upungufu wa vyumba vya madarasa vinane na sita viko katika hatua ya ukamilishaji huku walimu wakikosa vyoo vya uhakika na ofisi kwa ajili ya maandalizi ya masomo.

Akikabidhi matofali hayo jana, Mwenyekiti wa KACU Emmanuel Charahani, kwa Mkuu wa Wilaya ya Kahama Anamringi Macha, Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo Anderson Msumba alisema, lengo la utoaji wa matofali hayo ni kuunga juhudi za serikali katika kutatua changamoto ya miundombinu ya elimu.

Alisema, kiasi kilichotumia kununua tofauti hizo kinatokana na faida wanazozitapata wakati wa uuzwaji wa zao la tumbaku na pamba na kwamba wataendelea kusaidia pia katika ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali katika Halmashauri za Kahama mjini, Ushetu na Msalala.

"Ofisi yangu ilipokea barua kutoka kwa Mkurugenzi wa Kahama Mjini, Anderson Msumba, ikiomba kuchangia ujenzi wa vyumba vya madarasa msingi na sekondari, nilikaa kikao na bodi yangu tukakubaliana kuchangia tofali 2,000 na tutaendelea kuchangia na halmashauri nyingine za Ushetu na Msalala kupitia faida tunazozipata," alisema Charahani.

Akipokea tofali hizo, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Macha aliipongeza bodi ya KACU kwa kutoa tofali 2,000 ambazo zitakwenda kukamilisha vyumba sita vya madarasa vilivyo katika hatua ya ukamilishaji na kujenga vingine vipya kupunguza tatizo hilo.

Pia, Macha aliunga juhudi hizo kwa kuchangia mifuko 20 ya saruji shuleni hapo na kuwataka viongozi wa serikali za mitaa kuacha tabia ya kuwarubuni wananchi kutochangia ujenzi wa vyumba vya madarasa kuwa ujenzi huo unafanywa na serikali kabla hajaanza kuwachukulia hatua za kisheria.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Nyahanga, Benard Mapalala, alisema kuwa waliwahamasisha wananchi na wazazi kuchangia Sh. 5,000 kila kaya na kufanikiwa kujenga vyumba viwili na ofisi ya walimu moja katika Shule Nyahanga 'A' na bado wanaendelea na michango.

Alisema uchangishaji wananchi ujenzi wa madarasa kwa hiyari kwa sasa umekuwa mgumu baada ya kuibuka kwa kikundi cha watu kinachowahamasisha kutochangia kwa madai ujenzi huo unafanywa na serikali.




Mkuu wa Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, Selemani Mzee (Katikati), akimkabidhi godoro mmoja wa walimu wapya kati ya walimu 68, jana. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Walimu wapya wapatiwa magodoro kuanzia maisha

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WALIMU 68 walioripoti na kupangiwa vituo vya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara wamepatiwa magodoro 68 yenye thamani ya Sh. 6,080,000 kwa ajili ya kwenda kuanzia maisha wakati wakitekeleza majukumu yao.

Madogoro hayo walikabidhiwa jana mjini Masasi katika hafla fupi iliyoandaliwa na halmashauri hiyo, tukio lilihudhuriwa na Kaimu Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Ryoba Magabe, na Mkuu na Wilaya ya Masasi, Selemani Mzee kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa.

Akizungumza kabla ya kuwakabidhi magodoro hayo, Kaimu mkurugenzi huyo alisema, halmashauri imepokea walimu wapya 68 kwa ajili ya kufanya kazi katika halmashauri hiyo.

Alisema halmashauri imeshawapangia vituo vyao vya kazi na imeshaweka mazingira yote vizuri ya kufanyia kazi.

Magabe alisema mwezi Desemba, halmashauri ilipokea watumishi hao ikiwa ni ajira mpya iliyotolewa na serikali hivi karibuni.

"Halmashauri imeamua kuwapatia magodoro haya watumishi hawa ambayo thamani yake ni Sh. 6,080,000 ili wakaanze vyema maisha yao ya kiutumishi wakiwa na mazingira mazuri... tunaipongeza serikali kwa kutupatia watumishi hawa," alisema Magabe.

Akizungumza na watumishi hao, Mkuu wa Wilaya ya Masasi, aliwataka walimu hao kwenda kufanya kazi kwa kufuata kanuni na taratibu za utumishi wa umma na kufanya kazi kwa bidii.

Pia, aliwataka watumie fursa zilizopo katika maeneo yao ya kazi kwa kujiinua kiuchumi ikiwamo kumiliki ardhi kwa ajili ya kujenga makazi, kilimo na shughuli zingine za kiuchumi.

Alisema kusini kuna fursa nyingi za kiuchumi kama mashamba ya korosho na ufuta, na kuwataka walimu hao wazitumie fursa hizo pia kujiongezea kipato wakati wakiendelea na majukumu yao.

Wakizungumza na gazeti hili baadhi ya walimu hao kwa niaba ya watumishi wenzao, waliipongeza halmashauri kwa kuwapatia magodoro hayo na kuahidi kufanya kazi kwa kuzingatia miongozo ya utumishi wa umma.

Nipashe
Spotika




NYOTA 10 WENYE THAMANI KUBWA ZAIDI SOKONI 2021 UK. 12-13

# NYOTA WA5 WALIOBADILISHA NAMBA WAKAFITI




## ISIKUPITE

PHIL Foden ndiye mchezaji anayeongoza kwa kufunga mabao mengi zaidi Manchester City katika mashindano yote msimu huu akiwa na mabao tisa kwenye mechi 25 alizocheza, ikiwa ni bao moja zaidi ya aliyofunga katika mechi 38 msimu uliopita.



**LONDON,** England

KADRI miaka inavyokwenda kunaufanya mpira wa miguu kuwa bora zaidi. Idadi ya saa zinazotumika kwenye kujifunza nafasi nzuri ya kucheza ni sehemu ya wachezaji wa soka.

Wachezaji kadhaa hapo nyuma walibadilisha nafasi zao za kucheza kutoka zile walizoanza nazo. Bastian Schweinsteiger, kwa mfano, alianza kucheza kama winga wa kulia, kabla ya kubadilisha nafasi ya kucheza kiungo wa kati kwa Bayern Munich na Ujerumani.

Wachezaji kama Javier Mascherano, Steven Gerrard na Vincent Kompany wote walibadilisha nafasi zao za kucheza dimbani na baadaye wakawa wachezaji wakubwa na bora zaidi duniani.

Katika makala haya, tunawaangalia wanasoka watano ambao walibadilisha nafasi zao za kucheza na kuwa na mafanikio makubwa sana, twende sasa...

**#5. Alphonso Davies**

Alphonso Davies alianza kama winga wa kushoto kule Bayern Munich chini ya Hansi Flick msimu wa 2019-20, na alichukua nafasi hiyo kwa mikono miwili.

Kinda huyo wa Canada alikwenda Bayern akicheza kama winga wa kushoto. Hata hivyo, hakuwa anapata nafasi nyingi za kucheza hasa kutokana na uwapo wa Serge Gnabry, Franck Ribery na Kingsley Coman.

Bayern wakalazimika kumhamishia David Alaba kwenye nafasi ya mlinzi wa kati, kitu ambacho kiliwafanya wamhitaji mlinzi wa kushoto, huku Lucas Hernandez na Niklas Sule wakiwa wameumia kwa wakati huo.

Chini ya Flick, Davies akapewa nafasi kubwa na kucheza nafasi ya mlinzi wa kushoto kutokana na kasi yake.

Bayern ilijikuta ikitawala zaidi mechi zake kwani Davies alikuwa akipanda kama winga, licha ya kucheza nafasi ya mlinzi wa kushoto.

**#4. David Alaba**

Alaba mara zote amekuwa akijulikana kama mchezaji kiraka. Kwa miaka michache, alicheza kama mlinzi wa kushoto kwa Bayern Munich, huku pia akicheza kama kiungo wa kati kwa timu ya Taifa ya Austria.

Hata hivyo, kutokana na tatizo la majeruhi kuiandama Bayern Munich msimu uliopita, Alaba akalazimika kuzoea kucheza nafasi nyingine. Alifanya hivyo kwa urahisi tu, wakati Hansi Flick alipomchezesha na Jerome Boateng kwenye moyo wa ulinzi wa Bayern Munich.

Alaba ni mrefu wa kutosha, anasoma mpira vizuri, na yupo huru akiwa na mpira. Hivyo, kwa sura yake ni wazi kwamba inaonyesha amefiti zaidi kucheza nafasi ya mlinzi wa kati.

**#3. Dani Alves**

Dani Alves, wakati akitamba pale Barcelona, Juventus na Paris Saint-Germain alijijengea jina lake kama mlinzi bora wa kulia kuwahi kuucheza mpira.

Mchezaji ambaye amebeba mataji mengi zaidi kwenye soka, na Alves akajiunga na kilabu ya nchini kwao Brazil, Sao Paulo mwaka 2019, na alipewa jezi yenye namba 10. Na si kwamba hii ilikuwa kama Arsenal walipompa William Gallas jezi namba 10 wakati alipotua pale licha ya kuwa mlinzi wa kati.

Alves amebadilika yeye mwenyewe kwa sasa anacheza kama kiungo mshambuliaji kwa klabu hiyo ya Brazil, na haonyeshi ishara yoyote ya kuacha kucheza kwenye nafasi hiyo hivi karibuni.

**#2. Gareth Bale**

Bale alikuwa anacheza kama mlinzi wa kushoto wakati akiwa kwenye akademi ya Southampton, kabla ya kujiunga na Tottenham Hotspur. Na kule hakuendelea tena kucheza kama mlinzi wa kushoto.

Bale hakuwa na nafasi kwenye kikosi cha kwanza, wakati Harry Redknapp akaamua kutumia ubora wa raia huyo wa Wales katika nafasi nyingine kabisa na akaja kuwa mchezaji wa daraja la juu duniani.

Kiukweli, msimu wa 2012-2013, Bale alitwaa tuzo ya mchezaji bora wa mwaka kwenye Ligi Kuu England baada ya kuwa kwenye kiwango bora kabisa na Spurs, na ikamfanya asajiliwe na Real Madrid.

Kwa kawaida mambo huwa yanabadilika, lakini alifanya vizuri kwa kipindi kichache cha uchezaji na Los Blancos hao. Mabao mawili kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, bao dhidi ya Barcelona kwenye fainali ya Copa Del Rey - kumemfanya Bale kuwa kwenye kumbukumbu ya kudumu kwa mashabiki wa Real Madrid.

**#1. Sergio Ramos**

Hata wakati wa fainali za Kombe la Dunia mwaka 2010, Ramos alikuwa akicheza kama beki wa pembeni kulia kwa Hispania.

Lakini kwenye kikosi cha Real Madrid alikuwa akicheza kwenye moyo wa ulinzi wa pembeni kwa klabu hiyo. Lakini sasa hata kwenye kikosi cha timu ya taifa anacheza kama mlinzi wa kati ambapo pia ndio nahodha wa kikosi hicho.

# NYOTA 10 WENYE THAMANI KUBWA ZAIDI SOKONI 2021

**NYON,** Uswisi

KLABU za soka si sehemu tena ya burudani tu kwenye mtindo wa maisha, kwani sasa ni biashara kubwa zaidi. Kama ilivyokwa biashara nyingine, soka vitega uchumi vyake ni wachezaji wenye thamani kubwa. Tangu klabu kubwa duniani zikitengeneza mapato makubwa, wachezaji bora wanakuwa na thamani kubwa zaidi.

**Thamani ya mchezaji sokoni inaonyesha ni namna gani klabu inavyoweza kugharimu kiasi kikubwa cha fedha kumnunua mchezaji husika. Kuna sababu kadhaa ambazo zinachangia thamani ya mchezaji kuwa mkubwa sokoni, mojawapo ni mshahara wake, ubora wa uchezaji na mkataba.**

Sababu nyingine ya thamani kubwa kwa mchezaji sokoni ni hali ya soko husika. Kwa mfano thamani ya wachezaji ilipanda zaidi baada ya Neymar kusajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia wakati anatoka Barcelona kwenda Paris Saint-Germain Agosti mwaka 2017 kwa euro milioni 222.

Usajili ule ulileta athari kubwa zaidi kwenye soko, kwani wachezaji thamani yao ikazidi kupanda.

Mwingine? Cristiano Ronaldo - ambaye aliweka rekodi ya thamani kubwa duniani kufika euro milioni 120 mwaka 2014 na hapa hayupo kwenye orodha hii ya wachezaji 10 (ingawa alikuwa na thamani ya euro milioni 120 kwa mara nyingine tena mwaka 2018).

Makala haya yanawaangalia wachezaji 10 ambao wameweka rekodi ya thamani kubwa kwenye historia ya soko la wachezaji.

### #10. Philippe Coutinho – Euro Mil. 150

Thamani kubwa zaidi: ***Euro Mil. 150***
Rekodi iliwekwa: ***31/10/2018***
Thamani ya sasa sokoni: ***Euro Mil. 50***

Philippe Coutinho aliondoka Liverpool kwenda Barcelona Januari 2018, kwa ada iliyoripotiwa kuwa euro milioni 145. Hata hivyo, wakati huo, thamani yake sokoni ilikadiliwa kuwa euro milioni 90.

Alianza vizuri maisha pale Barcelona, akifunga mabao 10 katika mechi 22 kwenye mashindano yote mwishoni mwa msimu wa 2017-18. Matokeo yake kutokana na kiwango chake mwaka 2018, Coutinho aliweka rekodi ya thamani kubwa zaidi sokoni ya euro milioni 150, Desemba 2018.

Tangu hapo, Coutinho amekuwa na wakati mgumu dimbani na thamani yake sokoni imezidi kushuka, licha ya kuwa na mafanikio makubwa wakati akicheza kwa mkopo kule Bayern Munich msimu wa 2019-20 wakati alipowasaidia kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Akiwa amerudi Barcelona kuelekea msimu wa 2020-21, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, amecheza mechi 14 kwa Barcelona katika mashindano yote msimu huu, na thamani yake ya sasa sokoni ni euro milioni 50.

### #9. Kevin De Bruyne – Euro Mil. 150

Thamani kubwa zadi: ***Euro Mil. 150***
Rekodi iliwekwa: ***28/05/2018***
Thamani ya sasa sokoni: ***Euro Mil. 120***

Bila shaka ni mmoja wa viungo bora zaidi duniani kwa sasa, nyota huyu wa Manchester City, Kevin De Bruyne, bila shaka yoyote ana thamani zaidi ya euro milioni 100, huku thamani yake ya sasa inakadiriwa kuwa ni euro milioni 120.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 thamani yake kubwa zaidi sokoni ilikuwa ni euro milioni 150 ambayo aliiweka Mei mwaka 2018.

Kwa mwaka 2020, thamani yake ilishuka hadi euro milioni 120.

### #8. Antoine Griezmann – Euro Mil. 150

Thamani kubwa zaidi: ***Euro Mil. 150***
Rekodi iliwekwa: ***31/10/2018***
Thamani ya sasa sokoni: ***Euro Mil. 60***

Tangu alipohamia Barcelona, Antoine Griezmann amekuwa hayupo kwenye kiwango chake kama alivyokuwa kule Atletico Madrid na hiyo pia imefanya thamani yake kushuka. Griezmann aliweka rekodi yake ya thamani kubwa ya euro milioni 150 mwishoni mwa msimu wa 2018 wakati akicheza kule Atletico Madrid.

Alihamia Barcelona Julai 2019 kwa mkataba wa miaka mitano, lakini kiwango chake kikaporomoka. Griezmann alifunga mabao 24 tu katika mechi 72 kwenye mashindano yote kwa klabu hiyo ya Catalunya. Lakini katika misimu mitano aliyokuwa kule Atletico Madrid, alikuwa akifunga mabao 25 zaidi kwa kila msimu, ikiwa ni misimu minne mfululizo.

Kushuka kwa kiwango kwa Griezmann mwenye umri wa miaka 29 hapo Barcelona kumeathiri thamani yake sokoni na sasa inakadiriwa kuwa ni euro milioni 60.

### #7. Harry Kane – Euro Mil. 150

Thamani kubwa zaidi: ***Euro Mil. 150***
Rekodi iliwekwa: ***28/05/2018***
Thamani ya sasa sokoni: ***Euro Mil. 120***

Harry Kane ameendelea kuwa mmoja wa wachezaji wenye thamani kubwa zaidi duniani kwa zaidi ya miaka miwili sasa. Mmoja wa washambuliaji bora zaidi kwa sasa, na nyota huyo wa Tottenham Hotspur aliweka rekodi ya thamani kubwa sokoni ya euro milioni 150, Mei 2018 na aliendelea hivyo hadi mwishoni mwa mwaka 2019.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 27, kwa sasa thamani yake sokoni imeshuka hadi euro milioni 120. Katika msimu huu wa 2020-21, Kane amekuwa na kiwango kizuri linapokuja suala la kufuga na kutengeneza nafasi, akifunga mabao 19 na kutoa pasi za mwisho 14 katika mechi 27 kwenye mashindano yote.

### #6. Mohamed Salah – Euro Mil. 150

Thamani kubwa zaidi: ***Euro Mil. 150***
Rekodi iliwekwa: ***28/05/2018***
Thamani ya sasa sokoni: ***Euro Mil. 120***

Mohamed Salah alihamia Liverpool Juni 2017 kwa ada iliyotajwa kuwa euro milioni 42. Wakati huo huo, thamani yake sokoni ilikuwa inakadiriwa kuwa euro milioni 35. Katika msimu wake wa kwanza pale Liverpool, Salah alifunga mabao 44 na pasi za mwisho 16 katika mechi 52 kwenye mashindano yote. Na matokeo yake thamani yake ikapanda na kuwa euro milioni 150 Mei mwaka 2018.

Kwa sasa anacheza msimu wake wa nne pale Liverpool, na nyota huyo mwenye umri wa- miaka 28 tayari amefunga mabao 111 kwa klabu hiyo, akisaidia kubeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na lile la Ligi Kuu msimu uliopita. Salah mkataba wake unatarajiwa kumalizika mwaka 2023, thamani yake ya sasa ni euro milioni 120.

### #5. Sadio Mane – Euro Mil. 150

Thamani kubwa zaidi: ***Euro Mil. 150***
Rekodi iliwekwa: 1***0/12/2019***
Thamani ya sasa sokoni: ***Euro Mil. 120***

Mshambuliaji mwingine wa Liverpool, Sadio Mane mweye umri wa miaka 28, pia amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani

Mwishoni mwa mwaka 2019, Mane alitoa mchango mkubwa wakati Liverpool ikibeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na taji la Ligi Kuu ya England na msimu huo wa 2019-20 thamani yake sokoni ilipanda na kuwa euro milioni 150.

Hata hivyo, thamani ya sasa ya Mane ni euro milioni 120 na mkataba wake unamalizika Juni 2023.

### #4. Raheem Sterling – Euro Mil. 160

Thamani kubwa zaidi: ***Euro Mil. 160***
Rekodi iliwekwa: ***10/12/2019***
Thamani ya sasa sokoni: ***Euro Mil. 110***

Manchester City lishinda mataji mawili (Ligi Kuu England na Carabao) msimu wa 2017-18 na baadaye mataji matatu (Ligi Kuu, FA na Carabao) msimu wa 2018-19. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, alifunga mabao 23 na mabao 25 kwenye mashindano yote. Na msimu wa 2019-20 alifunga mabao 31 kwenye mashindano yote.

Oktoba mwaka 2017, thamani ya Sterling sokoni ilishuka na kuwa euro milioni 50, lakini ikapanda hadi euro milioni 160 Desemba 2019. Katika msimu huu, kiwango cha Sterling kimeshuka akiwa hafungi sana, akifunga mabao nane katika mashindano yote kwenye mechi 25 kwa Manchester City hadi sasa.

Mlipuko wa corona mwaka 2020 pia umepunguza thamani ya Sterling ambaye mkataba wake unamalizika Juni 2023 na hadi Desemba 2020 thamani yake ilikuwa ni euro milioni 110.

### #3. Lionel Messi – Euro Mil. 180

Thamani kubwa zaidi: ***Euro Mil. 180***
Rekodi iliwekwa: ***01/01/2018***
Thamani ya sasa sokoni: ***Euro Mil. 80***

Ni mmoja wa wachezaji bora zaidi kuwahi kutokea duniani, Lionel Messi, na aliweka rekodi ya thamani kubwa sokoni ya euro milioni 180 Januari 2018 - muda mfupi baada ya usajili wa Neymar kupandisha soko.

Tangu hapo Messi mwenye umri wa miaka 33, thamani yake sokoni imekuwa ikishuka hasa kutokana na umri wake na ukweli ni kwamba bado hajasaini mkataba mpya na Barcelona, ambapo wa sasa unamalizika kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Huku ikiwa imebaki miezi mitano kwenye mkataba wake wa sasa, thamani ya Messi sokoni inakadiriwa kuwa euro milioni 80.

### #2. Neymar – Euro Mil. 180

Thamani kubwa zaidi: ***Euro Mil. 180***
Rekodi iliwekwa: ***24/01/2018***
Thamani ya sasa sokoni: ***Euro Mil. 128***

Wakati Neymar alipokamilisha usajili wenye thamani ya euro milioni 222 kutoka kwa miamba wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Barcelona kwenda Paris Saint-Germain Agosti mwaka 2017, thamani yake sokoni ilikadiliwa kuwa euro milioni 100.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 ambaye bado hajasaini mkataba mpya na PSG kwa sasa thamani yake inakadiriwa kuwa euro milioni 128.

### #1. Kylian Mbappe – Euro Mil. 200

Thamani yake kubwa zaidi: ***Euro Mil. 200***
Rekodi iliwekwa: ***17/12/2018***
Thamani ya sasa sokoni: ***Euro Mil. 180***

Anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani kwa sasa, Kylian Mbappe, na ni Ronaldo Nazario tu ndio alifunga mabao zaidi ya 21 kuliko Mbappe katika umri wa miaka 22. Cristiano Ronaldo na Lionel Messi hawakuwa kufunga idadi hiyo ya mabao walipokuwa na umri huo.

Mbappe alijiunga na Paris Saint-Germain kwa mkopo akitokea Monaco, Agosti 2017, kabla ya kuuzwa moja kwa euro milioni 145.

Tangu alipowasili PSG, Mbappe amefunga mabao 131 na pasi za mwisho 75 katika mashindano yote kwenye mechi 207.

Mbappe bado hajasaini mkataba mpya na PSG na kwa sasa thamani yake inakadiriwa kuwa euro milioni 180.



NEYMAR

MBAPPE

## Nukuu


“Najua kwamba ilimchanganya kwa kutocheza. Njaa yake inatakiwa kuwa kubwa wakati atakapocheza tena soka. Mesut [Ozil] ni mtu anayehitaji mazingira mapya na naamini sehemu pekee itakayomfaa kwa sasa ni Uturuki, juu ya yote anaweza kugawa mipira ambayo mastraika wanaihitaji. Kama wakifanya hivyo, watakuwa na nafasi nzuri ya kushinda taji la ligi. Nitafuatilia hilo kwa karibu sana,” **Kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger.**



“Sijui, kama ukiniuliza, nitasema nataka kubaki hapa kadri itakavyowezekana, lakini nilisema kabla, majaliwa yapo mikononi mwa klabu, mara zote nataka kucheza kwa asilimia 100 kwa dakika zote, mimi nipo kwenye klabu hii na nataka kushinda mataji mengi kadri nitakavyoweza. Na nataka kujitoa kwa asilimia 100 kwa watu, ambao wamenipenda kwa muda wote,” **Mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah.**



“Niliwaweka mfukoni, Andres Iniesta na Sergio Busquets hakuna aliyefurukuta mbele yangu, ulikuwa mchezo bora sana katika maisha yangu ya soka, ”**Kiungo wa zamani wa Arsenal, Jack Wilshere, alipoulizwa kuhusu mechi dhidi ya timu hiyo na Barcelona mwaka 2011.**



Nipashe Spotika



Wachezaji wa Taifa Stars wakiwa mazoezini: **MPIGAPICHA WETU**

# TAIFA STARS YASHINDA NA REKODI ZA KUTISHA

**Na Adam Fungamwango**

BAO la dakika ya 66 lililofungwa na Farid Mussa, limeifanya timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars kushinda bao 1-0 dhidi ya Namibia kwenye mechi ya pili ya Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zinazofanyika nchini Cameroon.

**Ni bao ambalo limeweka hai matumaini ya Tanzania kuingia kwenye hatua ya robo fainali ya michuano hiyo kutoka Kundi D ambalo ipo na timu za Namibia, Guinea na Zambia.**

Kwa matokeo hayo, Taifa Stars inashika nafasi ya tatu, ikiwa na pointi tatu, huku timu za Guinea na Zambia zikiwa juu, kila mmoja ikiwa na pointi nne.

Kwenye mechi ya kwanza, Stars ilikubali kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Zambia na sasa imebakisha mechi moja tu dhidi ya Guinea kabla ya kukamilisha idadi ya mechi tatu kwenye kundi hilo. Stars inahitaji kushinda ili iweze kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo kwa mara ya kwanza.

Kwa ushindi ambao Taifa Stars imeupata kwenye mechi hiyo, imeweka rekodi kadhaa, ukilinganisha na miaka 22 iliyopita ambapo ilichezwa kwa mara ya kwanza michuano hiyo nchini Ivory Coast mwaka 2009.

### NI USHINDI WA PILI MICHUANO YA CHAN

Ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Namibia, pamoja na kwamba ni ushindi wa kwanza kwenye michuano hiyo, lakini ni ushindi wa pili kwenye michuano hiyo kwani mwaka 2009 ilishinda bao 1-0 dhidi ya wenyeji Ivory Coast kwenye mechi ya Kundi A.

Ilikuwa ni Februari 25, 2009, Stars ilipoitandika Ivory Coast bao 1-0, ambalo lilifungwa na Mrisho Ngassa dakika ya 36 na ndiyo ulikuwa ushindi pekee kwa Stars kwenye michuano hiyo kabla ya juzi kushinda tena katika michuano hiyo msimu huu.

### YAWEKA REKODI YA CHAN 2009

Baada ya kufungwa mabao 2-0 dhidi ya Zambia kwenye mechi ya ufunguzi, Stars ikashinda bao 1-0 kwenye mechi ya pili dhidi ya Namibia, imeweka rekodi kama ilivyofanya michuano iliyopita.

Mwaka 2009, ilipoanza fainali hizo kwa kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Senegal, lakini ilishinda bao 1-0 kwenye mechi ya pili dhidi ya Ivory Coast, kabla ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Zambia.

### FARID KAMA NGASSA

Farid Mussa, mchezaji ambaye kwa sasa anaichezea Yanga, ameweka rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza kwa Tanzania kufunga bao kwenye hatua hiyo ya fainali hizo baada ya Ngassa kufanya hivyo miaka 22 iliyopita.

Ngassa ambaye aliweka rekodi ya kufunga bao la kwanza kwa Stars kwenye michuano hiyo nchini Cameroon, naye pia alikuwa akiichezea Yanga wakati huo.

### STARS SASA MBABE WA NAMIBIA

Kwa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Namibia, timu ya Tanzania, Taifa Stars inaingia kwenye rekodi ya kuinyanyasa timu hiyo, ikiwa imeifunga mara mbili na sare mbili kwenye mechi zote nne ambazo wamekutana.

Mara ya kwanza timu hizo zilikutana Desemba 19, mwaka 1992 kwenye mechi za awali za Kombe la Dunia na Stars ikaichapa Namibia mabao 2-0 hapa hapa nchini.

Mechi ya pili ilichezwa mwaka 1997, Mei 31 kwenye michuano ya COSAFA na timu hizo zilitoka sare ya bila kufungana. Ilikuwa ni Machi 2, 2014 wakati wa mechi za kirafiki za kimataifa, timu hizo zilitoka sare ya kufungana bao 1-1, kabla ya kukutana kwenye mechi ya pili ya CHAN na Stars kushinda bao 1-0.

## JE, WAJUA?



KITENDO cha Southampton kumtoa bingwa mtetezi, Arsenal kwenye Kombe la FA, kinaifanya timu hiyo kuwatoa mabingwa watetezi kwenye mashindano kwa mara ya kwanza tangu ilipoifunga na kuitoa Tottenham katika mechi ya marudiano mwaka 1902. 'Saints' hao wamepoteza mara saba mechi zake za hivi karibuni za Kombe la FA dhidi ya mabingwa watetezi.





# Serikali yazindua mwongozo chanjo ya mifugo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imezindua mwongozo wa utoaji wa chanjo dhidi ya magonjwa ya mifugo nchini ili kudhibiti utoaji holela wa chanjo hiyo.

Uzinduzi huo ulifanywa mwishoni mwa wiki jijini hapa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, baada ya hivi karibuni kusimamisha kwa muda utoaji wa chanjo unaofanywa na halmashauri nchini kupitia kampuni walizoingia nazo mikataba.

Alisema alisimamisha huduma hiyo baada ya kubaini chanjo zinatolewa holela kwa mifugo bila kuwapo utaratibu sahihi na kusababisha madhara kwa mifugo na hasara kwa mfugaji.

"Serikali inaamini mwongozo huu utahakikisha sekta binafsi na umma zinajua haki na wajibu katika zoezi zima la utoaji wa chanjo na kuhakikisha afya ya mnyama inabaki salama," alisema.

Alisema mwongozo huo umeandaliwa na wadau 30 huku akisema wizara ipo tayari kupokea maoni ya wadau sehemu ambazo mwongozo utaonekana kuwa na upungufu ili kuurekebisha na kuufanya uwe bora zaidi.

"Lengo ni kuhakikisha afya ya mifugo nchini inalindwa na mfugaji kutopata hasara ya mifugo yake kufa au kupata madhara mengine yoyote baada ya kuchanjwa," alisema.

"Niwaombe sekta binafsi hasa wale mlio vizuri katika jambo hili la chanjo msiwe na wasiwasi hata mkiingia mikataba na halmashauri ili mradi muwe na sifa na vigezo ndiyo maana ya sisi tukatoa mwongozo ili tufanye kazi pamoja."

Aliagiza viongozi wa wizara, mamlaka za serikali za mitaa, watoa huduma za afya ya mifugo na sekretarieti za mikoa wazingatie maelekezo yaliyopo kwenye mwongozo huo na utekelezwe kwa kuzingatia kudhibiti magonjwa ya mifugo nchini.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, alisema mkoa huo utahakikisha yote ambayo Wizara ya Mifugo na Uvuvi inatamani yatokee katika sekta ya mifugo, mkoa uko tayari kuyasimamia ili yalete tija kwa taifa.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Pauline Gekul, alisema serikali inafanya jitihada mbalimbali za kupata masoko zaidi ya mazao ya mifugo yenye ubora ambayo yanachochewa na uwapo wa chanjo bora.

"Niwaombe popote huu waraka ulipo ukatusaidie ili malalamiko ya mnada umeharibika au wilaya nzima kutokuwa na josho, hayo malalamiko yafike mwisho, kupitia mapato mbalimbali ambayo halmashauri wamekuwa wakipata yakiwamo ya minada iliyopo kwenye wilaya hizo, wanapaswa kutenga fedha kwa ajili ya kuyakarabati," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji nchini, Jeremiah Wambura, aliomba wizara hiyo kuangalia vyema namna ya kuisimamia tasnia ya maziwa ili iwe na tija zaidi kwa taifa.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, akikata utepe kuashiria uzinduzi wa Mwongozo wa utoaji chanjo dhidi ya magonjwa ya mifugo kwa mfumo wa ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi iliyofanyika jijini Dodoma. **PICHA:AUGUSTA NJOJI**.

# Viongozi watakiwa kufuatilia miti iliyopandwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

VIONGOZI wa Halmashauri za Mkoa wa Dodoma, wameagizwa kujenga utaratibu wa kutembelea na kufuatilia maeneo yote yanayopandwa miti ili kuhakikisha inastawi na kuondokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alitoa agizo hilo jana alipokuwa akiongoza upandaji miti pembezoni mwa barabara katika Kata ya Mkonze, jijini hapa ulioratibiwa na Wakala wa Huduma ya Misitu (TFS).

Alisema mwitikio wa upandaji wa miti ni mzuri, lakini kama ufuatiliaji hautafanywa hakutakuwa na matokeo yaliyotarajiwa.

"Zoezi hili ni zuri sana, lakini kama hatufanyi ufuatiliaji zoezi hili halina maana, hakikisheni mnafuatilia maeneo yote yaliyopandwa miti ili kuona namna inavyoendelea,"alisema.

Hata hivyo, alionyesha kufurahishwa na wakazi wa mitaa ya Kata ya Mkonze kwa kujitoa kupanda miti na kuunda kamati ya kufuatilia miti hiyo na kuahidi kuwachangia Sh. 500,000.

"Nimesikia mmeunda umoja wenu kwa ajili ya kufuatilia miti iliyopandwa, ni jambo zuri sana na la mfano, na mimi nitawachangia laki tano katika umoja wenu," alisema.

Alisema serikali inawekeza miradi mingi katika Jiji la Dodoma na kwamba ni wajibu wa wananchi kupanda miti kwa wingi ili kupendezesha jiji hilo badala ya kuacha maeneo yakiwa makame.

Kadhalika, Dk. Mahenge akipanda miti kwenye eneo hilo alibaini korongo ambalo limekuwa kero kwa wananchi wa eneo hilo linalosababisha usumbufu hasa kipindi cha mvua kwa watumiaji wa vyombo vya moto.

Kufuatia hali hiyo, alitoa siku tano kwa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), Mkoa wa Dodoma, kurekebisha tatizo hilo na eneo lipitike na wananchi hao.

Mkuu wa Idara ya Mazingira na Udhibiti wa taka ngumu wa jijini hapa, Dickson Kimaro, alisema katika eneo hilo imepandwa miti 2,000.

# Kamati yaridhishwa maboresho ya OSHA

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Katiba na Sheria imeridhishwa na maboresho yaliyofanywa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), ikiwamo kufutwa kwa baadhi ya tozo zilizokuwa kero kwa wamiliki wengi wa sehemu za kazi.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Mohamed Mchengerwa, aliyasema hayo juzi alipokuwa akihitimisha kikao cha kamati hiyo kilichopokea na kujadili taarifa kuhusu miundo na majukumu ya Taasisi mbalimbali chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Alisema Wakala huo ambao upo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu maboresho yaliyofanyika yamechangia mwitikio mkubwa wa wadau katika kutekeleza Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya mwaka 2003.

"OSHA imefanya kazi kubwa katika kuimarisha masuala ya usalama na afya mahali pa kazi hapa nchini kupitia uboreshaji wa mifumo yake ya utendaji," alisema.

Alisema wajumbe wametumia kikao hicho kuweka mipango na mikakati ya kuendelea kuzishauri taasisi wanazozisimamia namna bora zaidi ya kuendelea kuboresha utendaji wake.

Akichangia kwenye kikao hicho, Mbunge wa Viti maalum, Asha Abdallah Juma, alipongeza wizara inayoshughulikia masuala ya kazi chini ya Waziri Jenista Mhagama pamoja taasisi zake za OSHA, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), kwa kufanya mageuzi makubwa katika mifumo na taratibu zake kiutendaji ambayo yameboresha huduma kwa wananchi.

"Tumeona jinsi ambavyo OSHA imejipanga kulinda nguvu kazi ya taifa letu," alisema.

## HABARI MBEYA

# Shule zote Mbarali zaagizwa kuwapa chakula wanafunzi

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, ameagiza shule zote za msingi na sekondari wilayani humo, kuanza utaratibu wa kutoa chakula ukiwa ni mkakati wa kuongeza ufaulu na kusaidia watoto kusoma kwa furaha.

Mfune alitoa maagizo hayo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Mbarali, ambapo alisema ili kufanikisha zoezi hilo, madiwani wanapaswa kulibeba na kulisimamia.

Alisema moja ya mambo yanayochangia wanafunzi kutofanya vizuri kwenye masomo yao ni kutokuwapo chakula mashuleni, hivyo alihamasisha viongozi mbalimbali wa kata, vijiji na madiwani kuanza utekelezaji wa agizo hilo.

"Viongozi wa kata, vijiji na madiwani kuanzia sasa hamasisheni wazazi na walezi kuchangia chakula mashuleni na zoezi hilo lianze mara moja ili watoto wetu waanze kula chakula shuleni... hatuna sababu ya kusubiri kwa sababu wazazi mna chakula cha kutosha, tunahitaji kuongeza ufaulu wilayani kwetu lakini kuwasaidia watoto wanaotoka kwenye mazingira magumu kusoma kwa furaha," alisema Mfune.

Katika hatua nyingine, Mfune aliwaomba madiwani kusimamia ukamilishaji wa vyumba vya madarasa na madawati kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza.

Alisema suala la wanafunzi kukaa chini kutokana na uhaba wa madawati halikubaliki, watoto wanatakiwa kusoma kwenye mazingira yatakayowawezesha kupata elimu bora.

"Pamoja na kuhamasisha hili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa tuna mpango wa kutengeneza viti na meza lakini madawati kwenye shule za msingi kwa sababu huku kuna uhaba mkubwa," alisema Mfune.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Twalibu Lubandamo, alisema wameweka mikakati kwa kushirikiana na watendaji kuchangisha michango ya lazima kwa wananchi kuchangia madawati na vyumba vya madarasa.

Alisema mpango huo utafanikiwa kwa kuwa wameanzisha ushindani wa kila kata ili atakayekamilisha mapema kupewa motisha huku wakitembelea kila Kata kuhamasisha ukamilishaji wa miundombinu hiyo.

Diwani wa Mahongole, Patrick Mwaisoba, aliunga mkono hoja ya Mkuu wa Wilaya kuhusu watoto kuanza kula chakula shuleni na kwamba tayari amekwisha kuanza kuhamasisha wazazi kuchangia.



Eneo la barabara ya Block T na Kabwe Kama jijini Mbeya ni maeneo yaliyoathirika na mvua zinazoendelea kunyesha na kuleta adha kwa vyombo vya usafiri na wasafiri.
. **PICHA: GRACE MWAKALINGA** .

# CBA Mbeya yaja na mpango wa ujenzi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE) Ndaki ya Mbeya, kimezindua Mpango wa ujenzi wa Chuo hicho ambacho kitajengwa katika Kata ya Iganzo ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya Mkoa wa Mbeya.

Akizungumzia mpango huo, Mkuu wa Chuo hicho, Profesa Emmanuel Mjema, alisema kwa sasa wanatumia majengo ya kukodi, hali inayosababisha usumbufu kwa wanafunzi na walimu katika upatikanaji wa elimu.

Alisema mpango huo unalenga kumaliza kabisa tatizo la miundombinu kwani kukamilika kwake kutasaidia huduma ya elimu kutolewa katika hali ya utulivu na muda muafaka kuliko ilivyo sasa.

Prpf. Mjema aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali ya 55 ya Chuo hicho na ya saba tangu kuanzishwa kwa Ndaki ya Mbeya.

"Hitaji la huduma hii ya elimu ya biashara kwa wananchi ni kubwa kutokana na ukosefu wa miundombinu ya kutolea huduma hiyo, tunalazimika kupokea wachache, tumekuja na suluhisho la kuduma ambalo ni ujenzi wa majengo yetu kule eneo la Iganzo kwenye mpango mkuu wetu wa ujenzi, inaonyesha kitakuwa ni chuo kikubwa ambacho kitakidhi mahitaji," alisema Prof. Mjema.

Aliongeza kuwa chuo hicho kina asilimia 48 ya watoto wa kike, na kwamba wengi wao wako kwenye umri chini ya miaka 20, hivyo wanahitaji uangalizi makini ili kuweza kutimiza ndoto zao.

Alisema katika kuwawezesha kupata elimu bora na kutimiza ndoto zao wameanzisha ujenzi hosteli kwa wasichana ili kuwasaidia kutotumia umbali mrefu kwenda chuoni kuliko ilivyo sasa ambapo wengi wamepanga na huenda usalama wao ukawa mdogo.

Mgeni rasmi katika mahafali hayo, Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ambaye pia ni Mbunge wa Mbeya Mjini, aliupongeza uongozi wa CBE kuja na mpango wa ujenzi wa chuo hicho.

Alisema kwa kushirikiana na Serikali watakuwa bega kwa bega katika kukamilisha ujenzi wa chuo hicho ambacho kitachukua eneo la ekari 54.5.

Alisema atashiriki katika harambee mbalimbali zitakazofanywa na chuo hicho, na kwamba atawahamasisha wadau wengine kuunga mkono juhudi hizo ili kutengeneza mazingira rafiki ya watoto kupata elimu bora na kufanikisha ndoto walizojiwekea.

Aidha, aliwashauri wahitimu wa kozi mbalimbali kuondoa dhana ya kuajiriwa, badala yake maarifa waliyoyapata wakayatumie kuwa wabunifu kwenye miradi na shughuli za kibiashara.

# 8,392 sasa waanza kidato cha kwanza

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

JUMLA ya wanafunzi 8,392 waliochaguliwa kidato cha kwanza katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya wameanza masomo baada ya uongozi wa Jiji kufikia hatua nzuri za kukamilisha vyumba 34.

Vyumba hivyo vya madarasa vilikuwa vinahitajika kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya wanafunzi hao.

Hayo yalisema jana na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Amede Ng'wanidako, wakati akizungumzia ujenzi wa vyumba vya madarsa kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza kuanza masomo.

Alisema awali wanafunzi 1,539 wa kidato cha kwanza ambao matokeo yao yalizuiliwa kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa, lakini kutokana na jitihada za Serikali kukamilisha madarasa sasa wameanza masomo.

"Ujenzi wa vyumba vya madarasa umefikia hatua nzuri na sasa wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wameanza masomo... tunaamini miundombinu ya elimu bado inaendelea kuboreshwa na watoto wetu watasoma kwenye mazingira ya utulivu," alisema Ng'wanidako.

Ofisa Elimu Idara ya Taaluma, Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Obed Pascal, alisema wiki ya kwanza tangu shule zifunguliwe wanafunzi wengi wameripoti, na kwamba walimu wamejipanga kuhakikisha wanawafundisha watoto ili kuongeza ufaulu na kuwaongezea maarifa.

Diwani wa Kata ya Iganzo, Daniel Mwanjoka, alisema Sekondari ya Iganzo jumla ya madarasa manne ambayo yanahitajika yamejengwa na kwamba kwa sasa wamekuwa na ziada a madarasa mengine ambayo wanaendelea kuyajenga ili kumaliza kabisa uhaba wa vyumba vya madarasa shuleni hapo.

Naye Diwani wa Kata ya Mwakibete, Lucas Mwampiki, aliwashukuru wananchi kwa muitikio kujitolea kujenga vyumba vya madarasa, na kwamba kazi inayoendelea sasa ni kuongeza matundu ya vyoo na chumba maalum kwa ajili ya watoto wa kike kujisitiri.

Alisema kiasi cha Sh. milioni tisa ambacho kilichangwa na wananchi wa Kata ya Mwakibete kitasaidia kuendelea kujenga vyumba vya madarasa na miundombinu mingine ya elimu katika Sekondari ya Mwakibete.



# Uandishi wa vitabu kuipaisha lugha ya Kiswahili

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamaganba John Kabudi, amesema uandishi wa vitabu vingi vya lugha ya Kiswahili utaifanya lugha hiyo kuwa bidhaa kwa nchi mbalimbali pamoja na kuongezeka wa watumiaji wa lugha hiyo na kuwa utambulisho wa mwafrika.

Aliyasema hayo juzi alipofanya mazungumzo na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, ofisini kwake Vuga, akiwa katika ziara ya siku tatu mjini Zanzibar.

Alisema uwapo wa Taasisi ya Kiswahili Zanzibar ndani ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), utasaidia kutoa wataalamu waliobobea zaidi katika lugha hiyo ndani na nje ya nchi.

Alisema Tanzania imefanikiwa kushawishi lugha ya Kiswahili, kutumika katika Jumuiya ya kiuchumi ya Jumuiya ya Ushirikiano wa Kimaendeleo wa nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), ikiwa ni agizo alilolitoa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, katika kuikuza lugha hiyo duniani.

Profesa Kabudi alisema, ushirikiano unaoendelea kwa nchi hizo hasa katika nyanja za kiuchumi ni dhahiri kuwa Tanzania inaendelea kuungwa mkono katika jitihada mbalimbali za maendeleo, akitoa mfano wa ziara ya Waziri wa Nchi za Nje wa China, aliyofanya hivi karibuni nchini Tanzania.

Alisema ziara hiyo imeonyesha kukubaliwa kwa ombi la Rais Magufuli, la kuisadia Zanzibar kwenye ujenzi wa kilomita 148.3 za barabara, ikiwa ni chachu ya kurahisisha miundombinu ya kukuza uchumi wa buluu visiwani humo.

Waziri Kabudi alimuomba Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kusimamia vyema mradi wa kituo cha kutotolea vifaranga vya samaki kiliopo Beit El Ras, ili kitoe huduma kwa mwambao mzima wa Afrika Mashariki na Kati, na kuahidi kuwa wizara yake itafanya mazungumzo na mabalozi mbalimbali, ili kukisaidia kituo hicho, na kukisimamia vyema kutafuta soko kimataifa.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Africa Mashariki Profesa Palamagamba Kabudi, akizungumza na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla Vuga, akiwa katika ziara ya siku tatu Zanzibar. **PICHA: MAKAMU WA PILI WA RAIS.**

Akizungumzia Sekta ya Uvuvi na Kilimo, alisema ni dhahiri serikali imeweka bayana kukuza uvuvi wa bahari kuu, kama ilivyoelezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025, na kueleza kuwa serikali imeahidi kuleta meli nane za uvuvi, nne kati ya hizo ni kwa ajili ya Zanzibar.

Akitoa shukrani, Makamu wa Pili, alimshukuru Profesa Kabudi kwa kuona umuhimu wa kumtembelea ofisini kwake na kumpongeza kwa kueteuliwa kushika nafasi hiyo kwa mara nyingine, huku akizungumzia imani ya Wazanzibari na Watanzania juu ya uteuzi wake.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Awamu ya Nane inafanya vyema katika utekelezaji wa majukumu yake chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Alisema mafanikio mengi yaliyopatikana katika awamu hii, na imani ya Wazanzibari kwa serikali zao zote mbili, na kumtaka Waziri Kabudi kufanya ziara kisiwani Pemba ili kujionea namna wananchi wa kisiwa hicho walivyokuwa na imani na serikali zao.

Mapema Waziri wa Nchi Ofsi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilish Dk. Khalid Salum Mohamed, alimshukuru Waziri Kabudi pamoja na watendaji wa wizara yake, kwa ziara ambayo wamefanya muda muafaka kwa kutembelea ofisi mbalimbali hapa Zanzibar, akieleza kuwa itaamsha hisia na moyo wa utendaji, hasa kwa mawaziri ambao wengi wao ni wageni katika majukumu hayo.

Aidha Dk. Khalid alisema wizara yake imedhamiria kuzimaliza changamoto zilizobaki za Muungano kwa kipindi kifupi, ili kuendana na kasi ya serikali zote mbili.

# Kamati za kusimamia viongozi zasaidia utendaji wa serikali

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

UWAPO wa kamati za kudumu zinazosimamia viongozi wakuu katika Baraza la Wawakilishi, umesaidia kurahisisha utendaji kazi wa serikali katika sekta mbalimbali nchini.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, alitoa kauli hiyo alipokutana na wajumbe wa kamati ya kudumu ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia viongozi wakuu, walipofika ofisini kwake Vuga kumsalimia.

Hemed alisema, imani kubwa kwa kamati katika utekelezaji wa majukumu yao wakionyesha kuongeza uwezo wa kufanya vyema katika kusimamia majukumu yao kwa maslahi ya taifa.

Alisema Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, imefarijika kwa ujio wa kamati hiyo iliyopata fursa ya kutembelea taasisi mbalimbali za ofisi na kuwaahidi kuendeleza ushirikiano ili majukumu ya kamati yaweze kamilika vyema.

Hemed aliwapongeza wajumbe wa kamati hiyo, kwa uwajibikaji wao, na kuwataka wawe tayari muda wote kuishauri na kuieleza ofisi yake ili kuendana na kasi ya awamu ya nane ya kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

Naye mjumbe wa kamati hiyo, ambaye pia ni Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, Machano Othman Said kwa niaba ya kamati hiyo, amempongeza Makamu wa Pili wa Rais kwa kuteuliwa kushika nafasi hiyo.

Kamati imeridhika na mtendaji mkuu huyo wa shughuli za serikali jinsi alivyoanza utendaji wake kwa kasi katika kusimamia mwelekeo wa awamu ya nane wa kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

# Taasisi za kiraia zapanda miti kuhifadhi mazingira

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Umwagiliaji, Mifugo na Maliasili zisizo rejesheka, Dk. Soud Nahoda Hassan, amesema Taasisi za kiraia nchini zina wajibu wa kuweka usafi na kuhifadhi mazingira.

Aliyasema hayo jana huko Kinazini katika bahari ya Mpiga duri-Kizingo wakati wa upandaji miti aina ya mikoko ulioandaliwa na taasisi za kiraia ya mjini hapa.

Alisema mazingira ya Zanzibar yatalindwa na Wazanzibari wenyewe na kuitaka jamii iwe na mwamko wa kuhifadhi na kulinda mazingira ili kupambana na mabadiliko ya tabia nchi yanayoikumba dunia.

Alisema mazingira ya bahari ya Kinazni, Mpigaduri na Kizingo, yameharibiwa kwa kuchimbwa mchanga kukata mikoko na kutupa taka ovyo bila kuzingatia athari ya uharibifu wa mazingira katika fukwe za bahari.

“Ukataji wa mikoko ya asili iliyopo baharini pamoja na uchimbaji mchanga kati fukwe, vitendo hivi havikubaliki na vinapaswa kukomeshwa mara moja, na hii inapelekea kutokea mabadiliko ya tabia nchi wananchi waache mara moja kufanya vitendo hivyo, mazingira yalindwe watu wasifanye wanavyotaka na iwapo atatokea mtu kuharibu kwa makusudi sheria zimuandame,” alisema.

Alizipongeza taasisi hizo kwa kubuni njia hiyo ya kutunza mazingira ya bahari kwa kupanda mikoko katika eneo hilo na kuwataka wadau wengine wa mazingira kushirikiana na serikali kuangalia namna bora itakayosaidia kuondoa uharibifu wa mazingira katika eneo hilo.

Pia, aliwataka wananchi wote wanaoishi karibu na maeneo ya fukwe au kufanya biashara katika maeneo hayo, kuyatunza mazingira yote ya fukwe kwa kuacha kutupa taka ovyo, kukata mikoko ya bahari kwa ajili ya kufanya kuni na kuacha tabia ya kuchimba mchanga.

“Wananchi ni jukumu letu sote kuhakikisha mazingira ya bahari na fukwe yanalindwa, kufanya uharibifu wa kimazingira katika fukwe ni kusababisha kuleta athari kubwa ikiwamo hata kuhama maji baharini na kuja katika makazi ya watu,” alisema.

Naye Mwenyekiti wa Tasisi ya Kupambana na Mabadiliko ya Tabianchi Zanzibar (ZACCA) Mahafudh Shaban Haji, alisema wanakusudia kupanda mikoko 50,000 na miti mingine 20,000 ili kupunguza mabadiliko ya tabia nchi visiwani hapo.

Taasisi mbalimbali za kiraia ikiwamo Taasisi ya Usafi ya Mwanakwerekwe (USAFI HUB), Taasisi ya Kupambana na Madiliko ya Tabianchi (ZACCA), Taasisi ya Habari na Vijana (MYCN) na Taasisi ya Kuhifadhi Mazingira Jozani (JECA), zimeshiriki katika upandaji miti na jumla ya mbegu 2,000 za mikoko zilipandwa eneo la Bahari ya Kinazini.

# NIT yaiomba China ujenzi chuo kikuu cha usafirishaji

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO Cha Taifa Cha Usafirishaji (NIT) kimeiomba serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kuharakisha mchakato wa kuanza ujenzi wa Chuo Kikuu Cha Usafirishaji baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu.

Mpango wa chuo hicho unahusisha pia vyuo vikuu vitano vya usafirishaji barani Afrika ambavyo vimo katika mkakati wa Serikali ya China wa kujenga au kuendeleza vyuo vya usafirishaji kwa hadhi ya chuo kikuu.

Akijibu maswali ya waandishi wa habari hivi karibuni wilayani Chato katika ziara ya Waziri wa Mambo ya Nje wa China, Wang Yi alipotembelea Tanzania, Mkuu wa NIT, Prof. Zacharia Mganilwa, alisema:

"Nimekuja kwenye ziara hii kuiomba Serikali ya China kupitia kwa Waziri Wang Yi mchakato huu wa ujenzi wa kukibadilisha chuo chetu kuwa Chuo kikuu uweze kwenda kasi kidogo, hivi sasa tumeshakamilisha upembuzi yakinifu ambapo chuo chetu kitakuwa kati ya moja ya vyuo vikubwa barani Afrika."

Prof. Mganilwa aliongezea: "Ujenzi wa Chuo hiki utagharimu zaidi ya Sh. bilioni 130 za Kitanzania na kitakuwa chuo bora kabisa kwa ukanda wa Afrika Mashariki na Kati."

Alisema kuwa kukamilika kwake kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza rasilimali watu katika miradi mikubwa ya usafirishaji, ambayo inaasisiwa na serikali ukiwamo ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) na miradi ya ujenzi wa meli pamoja na barabara.

"Upembuzi yakinifu uliofanywa na na Chuo Kikuu cha Southwest Jiaotong cha China ulimalizika tangu mwaka juzi 2018, tunatarajia kuona mradi wa ujenzi ukianza," alisema na kuendelea:

"Tumekubaliana chuo hiki kikuu cha usafirishaji kitakuwa na ndaki tano ndani yake pamoja na taasisi moja."

Mbali na kuwa na ndaki tano, kitakuwa na ofisi, maabara, vyumba vya mikutano maktaba na hosteli za wanafunzi.

"Kutokana na China kuwa na teknolojia za kisasa, tunatarajia kupokea mashine za kufundishia za teknolojioa ya juu hasa baada ya kukamilika kwa ujenzi wa chuo."

Prof Mganilwa alisema kupandishwa hadhi kwa NIT kuwa chuo kikuu ni muhimu sana kwa Watanzania kwa sababu nchi inahitaji wataalam zaidi wa uchukuzi na usafirishaji katika kukuza uchumi wa nchi.

Alisema kuwa kuwapo kwa Chuo Kikuu hicho pia kuzisaidia nchi jirani kama Kenya, Uganda, Kongo DRC, Burundi, Rwanda, Uganda, Malawi na Zambia ili na wao waweze kupata mafunzo.

Balozi wa China nchini, Wang Ke alimweleza Rais John Magufuli ilipomtembelea Ikulu Jijini Dar es Salaam kwamba China imeridhia kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa mradi huo.

Balozi Wang alieleza kuwa msaada huo ni sehemu ya misaada na miradi mbalimbali ambayo China inaitekeleza nchini yenye lengo la kuimarisha uhusiano na ushirikiano kati yake na Tanzania.

Mwakilishi wa Serikali ya China wa masuala ya uchumi na biashara, Lin Zhiyong, amewahi kutembelea eneo la mradi huo ambalo ni chuo cha NIT kilichopo Mabibo, jijini Dar es Salaam.



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, akipata maelezo ya Mradi wa Usindikaji wa Gesi asilia itakayotumika kwenye mabasi yaendayo kasi yaliyozoeleka kama mwendokasi katika kituo kinachoendelea kujengwa cha magari hayo kilichopo Ubungo jijini Dar-es-salaam ambacho awali kilikuwa ni kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watakiwa kuripoti wanaoozeshwa utotoni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WATOTO wilayani Shinyanga wamesisitizwa kutoa taarifa kwa viongozi wa serikali akiwamo mtendaji wa kata wanaposikia mwenzao anataka kuozeshwa na kukatishwa masomo ili hatua za haraka zichukuliwe.

Katibu wa Mpango Mkakati wa Serikali Kitaifa wa Kutokomeza Matukio ya Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Aisha Omari, alibainisha hayo juzi wakati wa uundwaji wa mabaraza ya watoto ngazi ya kijiji, kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kupaza sauti za kupinga ukatili.

Alisema watoto wanapaswa kuwa mstari wa mbele kupambana na ukatili kupitia kwenye mabaraza yao ya watoto kwa kutoa taarifa za vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa, ikiwamo kubaini njama za kutaka kuozeshwa ndoa za utotoni ili serikali ichukue hatua kuzuia vitendo hivyo.

"Mabaraza haya ya watoto ngazi ya kijiji ni muhimu sana, ambapo watoto watakuwa wakisikilizana shida zao wenyewe kupitia viongozi wao, na kisha kuziwasilisha kwa viongozi wa serikali akiwamo mtendaji wa kata, ili shida hizo zitafutiwe ufumbuzi mapema kabla ya kuharibu ndoto zao," alisema Omari.

Alisema katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga vitendo vya ukatili dhidi ya watoto ambavyo vinawasumbua ni pamoja na suala la mimba na ndoa za utotoni.

Kwa upande wake, mratibu wa mradi wa kupinga ukatili dhidi ya wanawake na watoto kutoka Shirika la Rafiki la SDO, mkoani Shinyanga, George Nyanda, alisema wamefadhili uundwaji wa mabaraza hayo ya watoto ngazi ya kijiji, kwa ufadhili wa Shirika la Women Fund Tanzania (WFT), ili kuongeza nguvu ya kupinga ukatili dhidi ya watoto.

# Ubungo wafurahia neema ya madawati

**Na Beatrice Moses**

WAZAZI katika Kata ya King'ongo, wilaya ya Ubungo jijini Dar es Salaam, wamefurahia neema ya madawati yaliyopelekewa katika Shule ya Msingi King'ong'o pamoja na Sekondari.

Madawati hayo yalitolewa na Benki ya NMB na kusema watoto wao hawatakaa tena chini.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wananchi na wazazi wa wanafunzi wanaosoma katika shule hizo mbili, walisema kwa muda mrefu asilimia kubwa ya wananfunzi walikuwa wakikaa chini kutokana na uhaba wa madawati, hivyo msaada huo ni neema kubwa kwao.

"Makaratasi.. tupa kule.. visalfetii tupa kulee," walikuwa wakiimba wazazi hao wakati Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Aboubakar Kunenge, akipokea madawati 150 kwa ajili ya shule ya King'ongo kutoka benki ya NMB.

"Kwanza tunamshukuru Rais Dk. John Magufuli kwa kutupazia sauti hadi sasa tunaona vyumba vya madarasa vinajengwa, maana yake msongamano wa wanafunzi utapungua; lakini pia tunaishukuru Benki ya NMB kwa msaada huu wa madawati, hatimaye watoto wetu sasa suruali na sketi zao zitabaki salama maana walikuwa wakikaa chini kwenye makaratai na matofali huku wengine wakikaa kwenye visalfeti," alisema Salma Said, mmoja wa wazazi ambao watoto wao wanasoma katika Shule ya Msingi King'ongo.

Kunenge alisema benki hiyo wamekuwa wadau wakubwa wa maendeleo katika Mkoa wa Dar es Salaam, wanahakikisha masuala ya afya, elimu na mambo mengine ya kijamii yanatimia kwa kufuata utashi wa Rais Magufuli.

"Leo tumepokea madawati 400 kwa ajili ya shule nne za Wilaya ya Ubungo, miongoni mwa shule hizo ni hii ya King'ongo ambako kuna ukarabati na utanuzi wa vyumba vya madarasa unaendelea kwa agizo la Rais Magufuli," alisema Kunenge.

Alibainisha kuwa viongozi wa mkoa huo watahakikisha wanatimiza maagizo yote yanayotolewa na viongozi wa juu wa nchi ili kuhakikisha wananchi wanaondokana na changamoto mbalimbali ikiwamo za elimu.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Isaya Makore, alisema NMB wamekuwa karibu nao wakati wote walipowahitaji katika kupata suluhu ya changamoto mbalimbali za masuala ya afya na elimu, hata katika suala la Shule ya Msingi King'ongo wameonyesha mfano bora.

## HABARI KIMATAIFA

# UN yataka haki elimu licha ya Covid-19

**Paris,** UFARANSA

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, amesema wakati dunia inaendelea kukabiliana na janga hili la Covid-19, elimu ni haki ya msingi yenye faida kwa umma wa kimataifa, ilindwe ili kuepuka athari kwa kizazi hiki.

Gutteres aliyasema hayo jana katika ujumbe wake maalum katika maadhimisho ya siku ya elimu ambayo huadhimishwa Januari 24, kila mwaka.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu na Utamaduni (UNESCO), katika ripoti ya kimataifa ya ufuatiliaji wa elimu, lilisema kufungwa kwa shule katika nchi 31, kumeathiri milioni 800 sawa na nusu ya wanafunzi wote duniani.

**Hatari ya watoto kuacha shule, inaathiri kwa kiasi kikubwa jamii, ufungaji wa shule ni lazima uwe suluhu ya mwisho na kufungua iwe kipaumbele.**

"Nawashukuru sana kwa ujasiri wao wakati wa janga hili la Covid-19 ambalo katika kilele chake lililazimisha karibu kila shule, taasisi na vyuo vikuu kufunga milango yake," alisema Gutteres.

"Ukivuruga elimu, umemvuruga kila kitu na kila mtu."

Aliongeza kuwa watoto na vijana milioni 258 hawakuhudhuria shule na asilimia kubwa ni wasichana, ingawa hali hiyo ilisababisha ubunifu katika njia za kujifunza, kusoma, pia kuleta mustakabali bora miongoni mwa watu walio katika jamii za mazingira magumu.

Guterres alisema bila shaka elimu ni msingi wa kupanua wigo wa fursa, kubadili uchumi, kupambana na hali ya kuvumiliana na kuilinda dunia na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), hayatafikiwa.

"Wakati dunia ikiendelea kukabiliana na janga hili la Covid-19, elimu ni haki ya msingi na faida ya umma wa kimataifa ni lazima ilindwe ili kuepuka zahma kubwa kwa kizazi hiki."

Alisema zaidi ya nusu ya watoto wa umri wa miaka 10 katika nchi za kipato cha chini cha wastani hawakuweza kujifunza na kusoma.

Mkurugenzi mkuu wa UNESCO, Audrey Azoulay, akizungumzia suala la kufunga shule alisema ufungaji shule wa muda mrefu umesababisha ongezeko la athari za kisaikolojia katika jamii hususan wanafunzi.

"Hatari ya watoto kuacha shule, inaathiri kwa kiasi kikubwa jamii, ufungaji wa shule ni lazima uwe suluhu ya mwisho na kufungua iwe kipaumbele," alisema Azoulay

Twakimu za UNESCO zinaonyesha, kabla ya janga hilo duniani, nchi moja pekee kati ya tano, ilionyesha usawa wa elimu kupitia ufadhili.

Pia takwimu hizo zilieleza kupunguzwa kwa masomo na kusoma kwa muda mfupi kulifanyika katika nchi 48, duniani.

Pia UNESCO, linasema corona itaongeza pengo la ufadhili kwenye elimu kwa theluthi moja na kufikia Dola bilioni 200 kwa mwaka, kwa nchi za kipato cha chini na kati sawa ana asilimia 40 ya gharama zote za elimu.

Shirika lilieleza kuwa katika nchi tofauti duniani, shule zilifungwa kwa miezi mitatu hadi mitano na nusu, sawa na wiki 14 hadi 22 tangu kuzuka kwa janga la Covid-19, mwaka juzi.

Kati ya nchi hizo ni Amerika ya Kusini na nchi za visiwa vya Caribbean na Ulaya. **UN**

## Mlanguzi mkubwa mihadarati Asia anaswa

**Amsterdam,** UHOLANZI

POLISI nchini Uholanzi wamemkamata anayesemekana kuwa kiongozi wa genge kubwa la ulanguzi wa mihadarati duniani, baada ya Australia kutoa kibali cha kukamatwa kwake.

Tse Chi Lop, Raia wa Canada mwenye asili ya China, inasemekana kuwa ndio kiongozi wa genge hilo, ambalo linamiliki karibu Dola bilioni 70 katika soko haramu la dawa za kulevya kote barani Asia.

Aliorodheshwa kama mmoja wa watoro wanaotafutwa.

Tse alikamatwa katika uwanja wa ndege wa Schiphol, Amsterdam.

Australia ilitaka, Tse, ahamishwe hadi nchini humo kukabiliana na mkono wa sheria.

Polisi nchini Australia inaamini kuwa kampuni ya mlanguzi huyo ambayo pia inafahamika kama Sam Gor Syndicate, ndio inayoingiza hadi asilimia 70 ya mihadarati nchini humo.

Mlanguzi huyo, 56, amekuwa akilinganishwa na mlanguzi wa Mexico Joaquin "El Chapo" Guzman kwa sababu ya ukubwa wa biashara yake haramu anayoendesha.

Polisi nchini Australia inasema kwamba, imekuwa ikimtafuta Tse, kwa zaidi ya miaka 10 kabla ya kukamatwa mwishoni mwa wiki, akisubiri kuingia katika ndege ya kwenda Canada.

Taarifa ya polisi ambayo haikutaja jina lake, ilisema kibali cha kukamatwa kwake kilitolewa mwaka 2019, huku polisi nchini Uholanzi wakifanyia kazi taarifa iliyotolewa na Interpol.

"Alikuwa kwenye orodha ya wanaotafutwa na alikuwa anazuiliwa kulingana na taarifa za shirika la ujasusi," Msemaji wa polisi Uholanzi amesema Ijumaa. **BBC**



Waokoaji wakiwa wamembeba mmoja kati ya wachimbaji madini aliyeokolewa baada ya kunasa zaidi ya wiki mbili katika mgodi wa dhahabu uliolipuka, akiingizwa katika gari la wagonjwa, jana, jijini Qixia, Mashariki mwa Jimbo la Shandong, China. **PICHA/Xinhua News Agency**

# Larry King akumbukwa kuipaisha CNN

**Los Angeles,** MAREKANI

RAIS wa Shirika la Habari CNN, nchini Marekani, Jeffrey Zucker amesema, Larry King (pichani) alichangia pakubwa katika kuliangazia kurunzi shirika hilo na kuliweka kwenye ramani ya kimataifa.

Zucker aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika ujumbe wa rambirambi, baada ya mtangazaji wa miaka mingi wa Marekani, Larry King kufariki dunia akiwa na miaka 87.

Larry King, alijipatia umaarufu mkubwa kwa kipindi chake cha televisheni cha 'Larry King Live', alifariki dunia mwishoni mwa wiki.

Kwa miaka 63, mwanahabari huyo alitangaza katika redio na televisheni na kuweka rekodi kwenye kitabu cha kumbukumbu cha 'Guiness World Book of



Records' kama mwenyeji wa kipindi kilichoendelea kwa muda mrefu zaidi kwa kituo kimoja cha televisheni.

Alijiunga na shirika la habari la CNN, mwaka 1985 na kuanzisha kipindi cha 'Larry King Live' kilichoendelea kwa miaka 25 hadi alipostaafu.

Larry King alifanya maelfu ya mahojiano na watu mashuhuri kote duniani wakiwemo marais, mawaziri wakuu, viongozi mbalimbali wa kisiasa na hata wasanii wa tabaka mbalimbali.

Baada ya kustaafu kutoka kwa kituo cha televisheni cha CNN mnamo mwaka wa 2010, alianzisha makala yake 'Larry King Now' ambayo yalipeperushwa kwa redio na vituo mbalimbali vya televisheni.

Wachambuzi wanamtaja kama aliyekuwa na ustadi wa kipekee wa utangazaji na aliyefanya mahojiano yake bila kuwashinikiza wageni, hivyo kuwafanya wajihisi huru na kuzungumza bila kujidhibiti.

Mavazi yake pia yalikuwa ya kipekee kwa kuwa, kila alipoonekana kwenye televisheni, alivaa saspenda za kuvutia, shati na tai zilizowiana.

Larry King, alilazwa kwenye hospitali ya Cedars -Sinai mapema mwezi Januari, 2021 akiugua ugonjwa wa Covid-19. **VOA**

# SUAREZ KUONGEZEWA MSHAHARA ATLETICO




**MADRID,** Hispania

NYOTA wa Atletico Madrid, Luis Suarez, anatajwa kuwa kwenye orodha ya wachezaji watakaoongezewa mshahara kwenye LaLiga baada ya kuendelea vema na maisha yake ya soka klabuni hapo.

Nyota huyu, ambaye ni raia wa Uruguay aliungana na kikosi cha Diego Simione akitokea Barcelona mwanzoni mwa msimu wa 2020/21, baada ya kuambiwa kuwa hakuwa kwenye mipango ya Ronald Koeman.

Licha ya kufikisha umri wa miaka 34 wikiendi hii, Suarez ameweza kuonyesha umuhimu wake kwa Simeone, akiwa na mabao 11 kwenye mechi zake 14 alizocheza.

Barcelona walikubaliana kusogeza mbele malipo yake alipoamua kuondoka klabuni hapo dakika za mwisho na kuripotiwa kuwa mshahara wake wa mwaka ukisalia kuwa euro millioni 14 kwa mwaka kule Madrid.

Hata hivyo, kwa mujibu wa ripoti kutoka Marca, mkataba wake ulikuwa unahusisha kipengele cha kuongezwa kwa mkataba ikiwa atafikisha mabao 15 ya ligi kwa wiki zijazo.

Nyota huyu anaonekana kuwa yupo kwenye mstari kuiifikia idadi hiyo wakati Atletico wakifukuzia taji lao la kwanza tangu mwaka 2014, huku kipengele kingine kikihusisha kufikisha mabao 20 ya ligi.

# Conte haifikirii AC Milan



**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte amesisitiza Inter Milan itaendelea kujiangalia yenyewe na si kuitanzama AC Milan baada ya kukosa nafasi ya kupaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Wiki moja baada ya kuifunga Juventus 2-0, Inter ilishindwa kuendelea mbele baada ya kutoka sare ya bila kufungana na Udinese, Jumamosi.

Kikosi cha Conte kilipiga mashuti 10 pale kwenye dimba la Dacia Arena - lakini kilishindwa kupata bao wakati Conte akilimwa kadi nyekundu dakika za majeruhi.

Milan ilichapwa mabao 3-0 na Atalanta Jumamosi hiyo, lakini Inter sasa imepitwa pointi mbili na vinara hao kwenye msimamo.

Nerazzurri hao sasa wameshinda katika mechi moja tu kati ya nne zilizopita za Serie A, wakitoka kushinda mechi nane mfululizo hapo awali, na Conte amekubali kunahitaji kujiimarisha.

"Kama mara zote nilivyosema, tunahitaji kufikiria kuhusu sisi wenyewe na si wengine, kama vile Milan. Tunatakiwa kujikita kwenye kujiimarisha kwa matokeo yetu," alisema akiiambia Sky Sport Italia.

"Tunajaribu kufanya kazi kufikia ubora wetu sisi wenyewe. Nafikiri hilo linawezekana kwa njia nyingi tu."

# De Beek hana furaha - Solskjaer

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema Donny van de Beek hana furaha hapo Old Trafford kutokana na kutopata muda mwingi wa kucheza.

Kiungo huyo wa kimataifa wa Uholanzi ameanza katika mechi tisa tu hapo United tangu alipojiunga akitokea Ajax kwa ada iliyoripotiwa kuwa pauni milioni 40, mbili kati yake zikiwa kwenye Ligi Kuu England.

Hajacheza katika mechi zote tatu zilizopita za United tangu kwenye mchezo wa FA wa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Watford Januari 9, lakini jana alitarajiwa kucheza dhidi ya Liverpool.

Solskjaer mwenyewe alikuwa na wakati mgumu wa kuanza mara kwa mara wakati wa siku zake za mwanzo chini ya Alex Ferguson na amemsifia Van de Beek kwa kuendelea kuwa mtulivu.

"Siwezi kusema Donny ana furaha," alisema. "Bila shaka, anataka kucheza zaidi, lakini hajapata nafasi hiyo.

"Hiyo inanikumbusha kuhusu mimi mwenyewe, wakati mara ya kwanza nilipofika hapa, na anaelewa wakati wake mgumu na changamoto zilizopo.

"Tunafanya vizuri na tumepata wachezaji ambao wanacheza vizuri kwenye nafasi zao.

"Ilikuwa hivyo hivyo kwa Sir Alex. Wakati aliponiacha nje na nilielewa na nilikuwa na furaha kwa ushindi wa timu na Donny ni mtu wa aina hiyo."

Van de Beek amecheza mechi 10 za Ligi Kuu kwa ujumla wake hapo United alifunga bao lake pekee kwenye ushindi wa 3-1 dhidi ya Crystal Palace, Septemba.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, bado hajatoa pasi ya mwisho yoyote hadi sasa.



## HABARI MICHEZO

# Benzema amtaja Hazard ubora Madrid

**MADRID,** Hispania

KARIM Benzema amemshauri Eden Hazard "kutengeneza jina lake" hapo Real Madrid, baada ya nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji kuonyesha kiwango cha kuvutia kwenye mchezo dhidi ya Deportivo Alaves, Jumamosi.

Hazard alifunga bao na akatengeneza moja kati ya mawili ya Benzema wakati Madrid ikiibuka na ushindi wa 4-1 dhidi ya wanaosuasua kwenye LaLiga, Alaves, na hivyo kupunguza presha kwa Zinedine Zidane, ambaye hakuwapo kwenye mchezo huo kwa sababu ana maambukizi ya virusi vya corona.

Madrid ilipoteza mechi zake mbili zilizopita, dhidi ya Athletic Bilbao kwenye Supercopa de Espana kabla ya kufungwa na Alcoyano kwenye Copa del Rey [Kombe la Mfalme]katikati ya wiki.

Casemiro alianza kwa kufunga bao la ufunguzi kabla ya Benzema kufunga mawili na Hazard moja ambalo ni la tatu kwenye msimu huu kwenye mashindano yote.

Hazard, alisajiliwa kutokea Chelsea mwaka 2019, na amekuwa kwenye kiwango kigumu kutokana na majeruhi mara kwa mara tangu atue hapo Madrid, lakini kwenye mchezo dhidi ya Alaves alionyesha kiwango chake bora kabisa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, sasa akiwa anaonyesha ishara ya "kufufuka", Benzema, ambaye amefunga mabao 10 ya ligi msimu huu, amemtaka Hazard kutengeneza jina lake kwa miamba hao wa Hispania.

"Mara zote napenda kuwasaidia wachezaji wenzangu," alisema Benzema akiiambia Movistar.

"Hazard nafikiri alikuwa mchezaji bora wakati akiwa mchezaji wa Chelsea na sasa anatakiwa kutengeneza jina lake hapa Madrid. Tunahitaji ubora wa Hazard."





# IBRAHIMOVIC: AC MILAN IMEFUNGWA KIRAHISI

**MILAN,** Italia

ZLATAN Ibrahimovic anahisi AC Milan "imevunjika kirahisi" na kutaka wajibu haraka kipigo cha mabao 3-0 walichokipata Jumamosi kutoka kwa Atalanta, wakati mchezo wao ujao utakuwa dhidi ya Inter Milan.

Awali walikuwa hawajafungwa katika mechi 27 kwenye ligi kuanzia msimu wa 2019-20, Milan sasa imepoteza mechi zake mbili zilizopita kati ya nne - pia walichapwa 3-1 na Juventus mapema mwezi huu.

Mabao kutoka kwa Cristian Romero, Josip Ilicic na Duvan Zapata yalikata kabisa ngebe za kocha, Stefano Pioli, lakini bado wanaongoza msimamo wa ligi baada ya wapinzani wao Inter kulazimishwa sare ya bila kufungana na Udinese.

Hata hivyo, Ibrahimovic amekubali kwamba, kama hawatajirekebisha, mambo yanaweza kuwa magumu kwenye mbio za kuwania taji la ligi.

"Tumepoteza mechi mbili baada ya zaidi ya mechi 30 bila kufungwa," alisema akiiambia Sky Sport Italia.

"Timu imevunjika kirahisi kwa sababu wakati wachezaji kadhaa wanakosekana, tunakosa uzoefu. Nafasi zao zinachukuliwa na wachezaji vijana, lakini hiyo si sababu.

"Tumejitolea kwa mengi; tunafanya kazi na tupo nafasi ya kwanza kwa sababu.

# *Wilshere afunguka kuwaficha Xavi, Iniesta*

**LONDON,** England

JACK Wilshere ametania kwamba, kuna wakati aliwashika viungo maarufu wa Barcelona, Andres Iniesta na Sergio Busquets na kuwaweka mfukoni mwake.

Wilshere alikuwa kwenye maswali na majibu kupitia ukurasa wake wa Twitter wakati alipoulizwa juu ya mechi dhidi ya Barcelona mwaka 2011, na alitania kwamba alitawala uwanja wa kati usiku huo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Arsenal.

Alicheza vizuri kweli, na Arsenal walifanikiwa kushinda 2-1 kwenye Uwanja wa Emirates katika mchezo wa kwanza wa hatua ya 16-bora kutokana na mabao ya Robin van Persie na Andrey Arshavin.

Wilshere alikuwa kijana tu wakati huo, na alionekana kuwa mmoja wa viungo wanaokuja juu barani Ulaya.

"Niliwaweka mfukoni, Andres Iniesta na Sergio Busquets hakuna aliyefurukuta mbele yangu, ulikuwa mchezo bora sana katika maisha yangu ya soka."

Alikuwa mchezaji kijana wa kwanza kabisa Arsenal Septemba 2008, akiwa na umri wa miaka 16 na siku 256, kucheza dhidi ya Blackburn Rovers.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# KLOPP ATULIZA PRESHA SALAH MKATABA MPYA

## Tunataka kuulizwa maswali na tunajibu, lakini suala la Mo haliko hivyo, sidhani kama...

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amesisitiza kwamba, mazungumzo ya mkataba mpya wa nyota wa Liverpool, Mohamed Salah, hayana kizuizi chochote kwa timu.

**Salah mkataba wake wa sasa pale Anfield unamalizika mwaka 2023, lakini majaliwa yake yamekuwa mjadala baada ya kukataa kuondoa uwezekano wa yeye kwenda Real Madrid au Barcelona wakati wa mahojiano yake na gazeti la AS mwezi uliopita.**

Huku Liverpool ikiwa kwenye kiwango kisichoridhisha na ikiwa nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu, Salah amefunga mabao 13 na kuwa kinara wa ufungaji hadi sasa kwenye mashindano hayo.

Kabla ya mchezo wa Kombe la FA wa jana Jumapili dhidi ya Manchester United, Klopp alisema hana shaka kuhusu Salah licha ya kuibuka kwa uvumi mwingi kuhusu majaliwa yake.

"Si suala la mchezaji kwenda nje na kujitolea kuzungumza kuhusu vitu ambavyo tunafikiri ni muhimu. Mara chache sana inatokea," alisema kocha huyo wa Liverpool akiwaambia waandishi wa habari.

"Tunataka kuulizwa maswali na baadaye tunajibu na hapo inaonekana kama ndio tumeanzisha mjadala mpya. "Lakini suala la Mo haliko hivyo, sidhani kama litakuwa na athari msimu huu."

Wakati Salah anaongoza kwa kufunga mabao kwenye Ligi Kuu akiwa ametikisa nyavu mara 13, matano kati yake amefunga kwa penalti.

Na hiyo imemfanya kuwa na wastani mzuri wa asilimia 64.3 ya kufunga mabao mengi zaidi tangu alipojiunga na Liverpool akitokea AS Roma mwaka 2017.

Liverpool imeshinda mchezo mmoja tu kati ya sita kabla ya mechi ya jana pale Old Trafford.

## ZISIKUPITE

### SOKRATIS KUTUA LAZIO

MLINZI wa Ugiriki, Sokratis Papastathopoulos mwenye umri wa miaka 32, anapanga kujiunga na klabu ya Lazio ya nchini Italia baada ya mkataba wake na Arsenal kusitishwa. ***(Gazzetta dello Sport, via Football Italia)***

### BARCA KWA AGUERO, ALABA

BARCELONA ina matumaini inaweza kumsajili straika wa Manchester City, Sergio Aguero, mwenye umri wa miaka 32, na mlinzi wa Bayern Munich, David, 28, kwenye usajili wa kipindi cha majira ya joto. ***(Mundo Deportivo, via Mail on Sunday)***

### DEMBELE AWINDWA EPL

CHELSEA na Manchester United zinafuatilia hali ya mkataba wa Ousmane Dembele pale Barcelona, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, akiwa amebakiwa na miezi 18 kwenye mkataba wake wa sasa pale Nou Camp. ***(Sport, via Metro)***

### RODGERS ATAJWA CHELSEA

KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers, ni moja ya jina ambalo Chelsea wanaweza kulifikiria kuwa kocha wao mpya, kama wakiamua kumfukuza Frank Lampard. ***(Daily Star on Sunday)***

### BENITEZ SASA ASAKA TIMU

KOCHA wa zamani wa Liverpool na Newcastle United, Rafael Benitez, angependa kurudi haraka kwenye kazi ya ukocha baada ya kuondoka klabu ya Dalian Professional ya nchini China, huku Napoli na Roma zikionyesha nia ya kumtaka Mhispania huyo mwenye umri wa miaka 60. ***(Sunday Times)***

### KOEMAN ATAKA USAJILI

KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman, anajua hali ya kiuchumi ya klabu ni mbaya, lakini amesema inatakiwa kusajili wachezaji ili kujiimarisha. ***(Goal)***

### MAJALIWA YA LINGARD

MANCHESTER United itafanya uamuzi kuhusu majaliwa ya kiungo wa England, Jesse Lingard, 28, baada ya mchezo wa jana wa FA dhidi ya Liverpool, huku Newcastle United, Sheffield United na West Brom zikionyesha nia ya kumsajili kwa mkopo. ***(Mail on Sunday)***

### WEST HAM YAMTAKA EN-NESYRI

WEST Ham imehusishwa na straika wa Morocco, Youssef En-Nesyri, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, hataondoka Sevilla Januari hii. ***(Estadio Deportivo, via Sport Witness)***

### VILLA YAMPANDIA DAU SANSON

ASNTON Villa imeandaa ofa ya pauni milioni 15.5 kwa ajili ya kumsajili kiungo wa Marseille, Morgan Sanson mwenye umri wa miaka 26 raia wa Ufaransa. ***(Mail on Sunday)***

### EMERSON HUYO CHELSEA

CHELSEA imeipiku West Ham katika mbio za kuwania kumsajili kwa mkopo mlinzi wa Italia mwenye umri wa miaka 26, Emerson Palmieri. ***(Sunday Mirror)***

## HABARI MICHEZO

## Malale ageukia za kujipima Polisi

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la Klabu ya Polisi Tanzania, limesema linatafuta michezo ya kirafiki kwa ajili ya kujiandaa na mzunguko wa lala salama wa Ligi Kuu utakaoanza Februari 13, mwaka huu, pamoja na Kombe la Shirikisho maafuru FA Cup.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Malale Hamsini, alisema kikosi chake kimerejea kambini ili kujiweka sawa na mashindano hayo.

"Kikosi kimerudi kambini kwa ajili ya kujiandaa na mashindano yaliyopo mbele yetu, lengo ni kuiweka mahali pazuri klabu yetu," alisema Malale.

Alisema atahakikisha anawapa mazoezi magumu wachezaji wake ikiwa ni pamoja na kusisitiza nidhamu kwa kila mchezaji huku akiendelea kurekebisha makosa yaliyojitokeza mzunguko wa kwanza kwa kuwa anatarajia raundi ya pili ya ligi hiyo itakuwa ngumu zaidi.

## Tenisi kutimua vumbi Mei huko Cameroon

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya mchezo wa tenesi kwa timu za wakubwa ( Seniors) ya yanatarajiwa kufanyika mwanzoni mwa Mei mwaka huu nchini Cameroon, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Chama cha Tenesi Tanzania (TTTA), Leonard Liunda, alisema maandalizi kuelekea kwenye mashindano hayo yanaendelea vizuri.

Alisema mashindano hayo yatashirikisha nchi mbalimbali na kuwataka wachezaji wao kufanya mazoezi kwa bidii ili kufanya vizuri katika mtanange huo.

"Maandalizi ya mashindano hayo yanaendelea vizuri wachezaji wanafanya mazoezi kila siku ili waende kuiwakilisha nchi yetu," alisema Liunda.

Aidha, aliwaomba wadau wa mchezo huo waendelee kuwapa ushirikiano huku akiziomba taasisi na kampuni mbalimbali kujitokeza kuwaunga mkono.

Alisema kabla ya mashindano hayo kutakuwa na mashindano mengine ambayo yatawasaidia kuwaweka vizuri zaidi kuelekea katika mashindano hayo.

# MKUDE ASHUSHIWA RUNGU SIMBA, MAKOSA YAANIKWA

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE baada ya kimya cha muda mrefu sasa, Kamati ya Nidhamu ya Klabu ya Simba chini ya Mwenyekiti wake, Suleiman Kova, imetangaza makosa na hukumu ya Sh. milioni mbili kwa kiungo wa klabu hiyo, Jonas Mkude, ambaye alisimamishwa na uongozi kwa tuhuma za utovu wa nidhamu.

Akitangaza makosa hayo, Kova alisema Mkude amekutwa na makosa matatu aliyokuwa akituhumiwa kuyafanya, huku pia akiweka hadharani hukumu zake.

**Kosa la kwanza, Kova alisema lilikuwa ni kutohudhuria semina elekezi iliyohusisha wachezaji, benchi la ufundi na viongozi, ambayo adhabu yake ni faini ya Sh.milioni moja.**

Kova alisema kosa la pili ni kuchelewa kuingia kambini wakati timu ilipokuwa ikijiandaa na mchezo dhidi ya Coastal Union, adhabu aliyopewa ni karipio kali na faini ya Sh. milioni moja pamoja na kuwekwa katika kipindi cha uangalizi cha miezi sita.

Kosa la tatu, alisema ni kutoripoti kambini Desemba 26, mwaka jana bila ruhusa yoyote, ambapo katika tuhuma hizo, kamati haikumkuta na hatia baada ya kutothibitisha pasipo shaka shitaka hilo.

Aidha, kamati hiyo imemtaka Mkude kurejea kambini mara moja kuendelea na mazoezi na asipofanya hivyo atakuwa amefanya tena kosa la utovu wa nidhamu huku faini aliyotozwa akitakiwa kuilipa ndanI ya mwezi mmoja.

Lakini pia kamati hiyo imemtaka Mkude kuomba radhi kwa maandishi ndani ya saa 24 kuanzia jana.




Mshindi wa jumla wa mashindano ya Johnnie Walker Waitara Trophy, Khalid Shemndolwa (wa kwanza kushoto), akikabidhiwa zawadi ya vikombe baada ya kushinda. Wa kwanza kulia ni mwakilishi kutoka Resolution Insurance akifuatiwa na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama nchini, General Vanance Mabeyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Faraji Mnyepe, na Mkuu wa Majeshi wa Malawi, Generali Vincent Nundwe. Hafla hiyo ilifanyika jijini Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

# *Waziri Tabia awafunda wasanii Z'bar*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo wa Zanzibar, Tabia Maulid Mwita, amewataka wasanii wa Zanzibar kuwa wabunifu katika kazi zao ili kukuza na kuinua vipaji katika tasnia hiyo hapa nchini.

Waziri Tabia aliyasema hayo katika Ukumbi wa Sanaa Raha jana wakati alipokutana na wasanii mbalimbali visiwani hapa kusikiliza changamoto zinazowakabili katika kazi zao ili kuzitafutia ufumbuzi na kufikia malengo waliyokusudia.

Alisema wasanii wa Zanzibar licha ya kujitahidi katika kazi mbalimbali, wanashindwa kufikia malengo yao kwa sababu ya kutokuwa wabunifu wa kubuni mbinu mpya na za kisasa za kuendeleza fani hiyo kama ilivyo kwa nchi nyingine.

Tabia alisema kwa sasa dunia inatumia teknolojia katika kukuza mambo mbalimbali ikiwamo kazi za wasanii hivyo akawataka kuangalia namna bora ya kukuza kazi zao na kwa kuzifanya kutambulika duniani.

Alisema ni vema wasanii wa Zanzibar kwa pamoja wakabuni njia ambayo itasaidia kutangaza soko la sanaa hapa nchini.

Aidha, alisema katika kutatua changamoto zinazowakabili wasanii wa Zanzibar, serikali itashirikiana nao ili kubuni mbinu ambazo zitasaidia kufikia malengo ya kuinua vipaji vya sanaa ikiwa ni njia mojawapo ya kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi, CCM.

"Kaeni kwa pamoja mshirikiane, msibaguane wala msidharauliane, pangeni kitu halafu mtuletee sisi wizara tutakusaidieni ili muinue sanaa zenu msije mmoja mmoja mtakuwa hamfikii malengo," Waziri Tabia alisema.

Akizungumzia suala la utendaji, waziri huyo amewataka watendaji wa sekta husika kusimamia na kufuatilia majukumu yao ipasavyo kwa kukaa na wasanii wao ili kuondoa malalamiko na kufufua vikundi vya wizara ambavyo kwa sasa havipo tena.

Hata hivyo, ameahidi kuzifanyia kazi changamoto zinazowakabili wasanii pamoja na kuandaa kanuni maalum zitakazoweza kutanua soko la sanaa ndani na nje ya nchi.

Wakitoa malalamiko yao, wasanii kutoka vikundi mbalimbali wameiomba serikali kuweka mfuko maalum utakaowasadia katika kutatua baadhi ya matatizo yao.

Michezo

Jumatatu Januari 25, 2021

Nipashe



HABARI UK.20

## Suarez kuongezewa mshahara Atletico

# Ndayiragije ataja siri ya ushindi Stars

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Namibia, Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije, amesema huo ni muendelezo wa kazi ambao walishauanza na kuwataka Watanzania watarajie makubwa, lakini wasiwe na haraka.

Akizungumza baada ya mechi hiyo nchini Cameroon, kocha huyo raia wa Burundi, alisema wengi wanadhani kuwa Stars imeshinda baada ya yeye kufanya mabadiliko ya baadhi ya wachezaji, lakini ukweli ni kwamba kazi ya kuitengeneza timu hiyo inaendelea kila siku na ndiyo maana inaonekana kubadilika siku hadi siku.

Kwenye mechi dhidi ya Namibia, Stars ilianza na wachezaji ambao hawakucheza mchezo wa kwanza dhidi ya Zambia na wengine waliingia kipindi cha pili kama vile Said Ndemla, Deus Kaseke na Farid Mussa ambaye ndiye alifunga bao pekee dhidi ya Namibia.

"Ni kweli kulikuwa na mabadiliko ya wachezaji, lakini hiyo haimaanishi kwa asilimia kubwa ndiyo sababu ya kushinda ingawa kwa kiasi inawezekana, ila ushindi unatokana na muendelezo wa kazi ambayo inaendelea. Kuna kazi ya kukijenga kikosi ambayo inaendelea, lakini pia kufanyia kazi upungufu uliopo," alisema Ndayiragije.

Akizungumzia mechi ya mwisho dhidio ya Guinea ambayo kama Stars itashinda, itakwenda moja kwa moja hatua ya robo fainali, alisema kuwa ameshaanza kazi ya kuisoma timu hiyo.

"Haya ni mashindano na ni ya kutafuta ushindi, naenda kuwasoma wapinzani ili niangalie jinsi gani na kupambana nao," alisema.

# DIDIER AMRITHI SVEN SIMBA

●●● Ni Mfaransa aliyeitema Al-Merrikh, amtaja Kagere akitangaza makubwa Ligi ya Mabingwa na falsafa ya soka biriani kama...




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez (kulia), akimtambulisha na kumkabithi jezi Kocha Mkuu mpya wa klabu hiyo, Mfaransa Didier Gomes Da Rosa, jana jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Ofisa Habari wa klabu hiyo, Haji Manara. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**Na Saada Akida**

BAADA ya mchujo mkali wa makocha zaidi ya 70 walioomba kazi ya kurithi mikoba ya aliyekuwa Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, hatimaye uongozi wa klabu hiyo umemtangaza rasmi, Mfaransa Didier Gomes Da Rosa kuvaa viatu vya Mbelgiji huyo ambaye aliachia ngazi hivi karibuni baada ya kuipeleka timu hiyo hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kama ilivyo kwa Sven, Didier ambaye alikuwa Kocha Mkuu wa Al-Merrikh ya Sudan iliyopangwa kundi moja na Simba, naye aliachia ngazi baada ya kuiongoza timu hiyo kufuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa msimu huu.

Didier ambaye jana alisaini mkataba wa miaka miwili na Simba katika Hoteli ya Serena jijini Dar es Salaam na kuelekea Uwanja Mo Simba Arena, Bunju kuanza kazi ya kuinoa timu hiyo, amesema ni mwenye furaha kujiunga na mabingwa hao wa nchi na anaamini watafanya vizuri katika michuano iliyopo mbele yao.

Alisema ana fahamu soka la Tanzania ambalo linazidi kukua kila mwaka baada ya kulifuatilia kwa sababu amekuwa na utamaduni wa kufuatilia ligi za nchini mbalimbali hasa za Afrika.

"Pia Simba nimeifuatilia muda mrefu kabla ya kuomba kazi, kwa sababu ya Meddie Kagere ambaye alikuwa mchezaji wangu kipindi nafundisha Rayon Sports ya Rwanda.

"Falsafa yangu inaendana kidogo na soka la Simba, lakini naamini nitakutana na changamoto kubwa ya kuhakikisha nafanya vizuri kwa kuanza kushinda katika mechi zijazo za ligi (viporo) na kupambana kuvuka katika hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa," alisema Didier.

Alisema kundi la walilopangiwa Simba katika michuano hiyo ambalo linazijumuisha timu ya Al Ahly ya Misri, AS Vita ya DR Congo na Al-Merrikh ni gumu.

"Inakutana na timu zote nzuri, lakini ninaamini Simba iko vizuri pia, ina wachezaji wazuri tutafikia malengo ambayo yanayatarajiwa katika michuano hiyo," alisema Didier.

Kuhusu kutodumu kwenye timu anazozifundisha, alisema hilo ni jambo la kawaida kwa makocha na kwamba hutokana na changamoto wanazokutana nazo, lakini atahakikisha ndani ya Simba atamaliza muda wake na kufikia malengo yanayotarajiwa na Wanasimba.

"Nimefurahi kujiunga na Simba, ni timu kubwa na inashiriki michuano ya kimataifa, hivyo niwaondoe hofu mashabiki na viongozi, sitaondoka hadi muda wangu wa mkataba na nitapambana kufanya vizuri kutetea ubingwa na kuvuka makundi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Didier ambaye ameifundisha Rayon Sports (2013-2014) Coton Sport ya Cameroon (2014-2015) CS Constantine ya Algeria(2015-2016), JSM Skikda ya Algeria (2016-2017), Ethiopian Coffee (2017-2018), Horoya AC ya Guinea (2019), Ismaily ya Misri (2019-2020) na Al-Merrikh mwaka 2020.

Kwa upande wa suala zima la nidhamu katika timu anayoifundisha Didier alisema: "Hatuwezi kushinda na kuchukuwa mataji bila ya kuwapo kwa nidhamu, nitawapenda wachezaji wangu na kuwasisitiza suala hilo la nidhamu kwenye timu."

Naye Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema walipokea maombi ya kutoka kwa makocha 70 na baada ya mchakato, wameridhishwa na uwezo wa Didier na wameingia naye mkataba wa miaka miwili na jana alianza kazi moja kwa moja.

"Kocha ataendelea kufanya kazi akisaidiana na Selemani Matola ambaye tulikuwa naye tangu awali, kuhusu kocha wa makipa [Mbrazil Milton Nienov] hakuwa sehemu ya mipango ya kocha Didier kwani wakati tukianza mazungumzo na kocha tulikuwa na Sven, hivyo kila kitu kiliendা vizuri na hatukuweza kuachana naye," alisema Barbara.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >